# Ubora wa Maudhui ya Vyombo vya Habari Tanzania

## Ziko wapi sauti za wagombea na wananchi?

**UCHUNGUZI WA URIPOTI WA VITUO VYA REDIO KUHUSU UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2024 NCHINI TANZANIA**



RIPOTI
2024

**WATAFITI**

Dr Zacharia Malima
UDSM (SJMC)

Christoph Spurk
Spurk Media Consulting Ltd
Winterthur, Switzerland

Abdallah Katunzi
UDSM (SJMC)

Dr Darius Mukiza
UDSM (SJMC)

Emmanuel Ngabo
UDSM (SJMC)

**WAFASIRI**
Prof Michael Andindilile
University of Dar es Salaam
School of Journalism and Mass Communication

Prof. Ndeti Ndati
University of Nairobi (UoN)

**MSANIFU KURASA**
Essy Ogunde

**MSANIFU WA PICHA**
Halili Letea

ISBN 978 99 87 710 70 6
All rights reserved.

**Report Published by:**
Chup Kikuu cha Dar es Salaam
Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma
S.L.P  4067 Mikocheni B Makaburi Street, Plot Block D, No.34
Tel: +255 (22) 2700756 Dar es Salaam, Tanzania
Email: sjmc@udsm.ac.tz  yearbookmediatz@gmail.com

# Yaliyomo

Shukrani.................... ........................................................................................................ iii
Muhtasari Mahsusi........................................................................................................................ iv
1.0 Utangulizi.................................................................................................................................. 01
2.0Usuli - Mfumo wa Siasa wa Tanzania ........................................................................... 01
3.0 Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024............................................... ... 01
4.0 MATOKEO YA UTAFITI......................................................................................... 13
4.2 NGAZI YA 2: Matokeo kwa vituo vya redio vyenye leseni za wilaya, mkoa na za kijamii ............................................................................................................... 33
11.0 TIER 3: Results for the National Broadcaster—TBC Taifa..................................... 42
12.0 UFUATILIAJI WA WAKATI HALISI............................................................................ 42
3.0 MITAZAMO YA WADAU KUHUSU MATOKEO YA UTAFITI HUU...................... 44
14.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO................................................................................ 46

# Shukrani

Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM-SJMC) inazishukuru Balozi za Uswisi na Uingereza nchini Tanzania kwa msaada wao wa kifedha ulioelekezwa kwenye kuuunga mkono mradi huu wa Yearbook kuhusu ***"Ubora wa Maudhui ya Vyombo vya Habari Tanzania 2024***", na kwa dhamira yao isiyoyumba ya kuboresha ubora wa vyombo vya habari na uandishi wa habari nchini, jambo ambalo limeleta uaminifu, matunda na uendelevu wa mradi huu. Tunaishukuru sekta nzima ya habari nchini kwa kuendelea kuunga mkono mradi huu ambao kwa kiasi kikubwa umechangia kuboresha utendaji wa kiweledi nchini. Tunawashukuru wote waliotenga muda wao ili kushiriki mahojiano kwa uwazi na kwa upana zaidi kwenye mjadala kuhusu uripoti wa vituo vya redio kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024.

Mbali na hilo, tunawashukuru wataalamu walioipitia kazi hii, Prof. Michael Andindilile kutoka Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM-SJMC) na Prof. Ndeti Ndati kutoka Chuo Kikuu cha Nairobi (UoN).

Pia tunawiwa kuwashukuru watafiti wasaidizi wa utafiti huu kwa kujitolea kwao kwenye mradi huu: Theodora Munisi, Salma Tanzilu, Khalila Shaban, Theodora Theodory, Faidha Ngaga, Pascael George, Safina Yasini, Swaum Manengelo, Jackson Gilbert, Aisha Makame, Shadida Salum, Esther Kasanga, Teddy Mparanyanga, Caroline Malewo, Mwambelo Maiki Denson, Selina Luhizo, Benjamin Chisele, na Lineth Renatus. Kwa ujumla wao, walifanikisha mchakato mzima wa usimbuaji na uandishi wa taarifa zilizokusanywa kutoka kwenye vituo vya redio.

# Muhtasari Mahsusi

Utafiti wa Yearbook kuhusu "Ubora wa Maudhui ya Vyombo vya Habari Tanzania 2024 ulichunguza uripoti wa vyombo vya habari kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kwa kutumia vigezo mahsusi, utafiti huu ulivichunguza vituo 35 vya redio kutoka pande zote nchini Tanzania ukijumuisha vituo vya redio vya ndani vyenye leseni za mikoa, wilaya na redio za jamii pamoja na kituo cha Utangazaji cha Taifa (TBC Taifa).

Vigezo hivyo ni pamoja na jinsi walivyowahabarisha vizuri wananchi kuhusu uchaguzi na wagombea wa nafasi mbalimbali, jinsi walivyozihoji ahadi za wagombea na jinsi walivyowashirikisha wananchi (wapiga kura) ambao kwa mujibu wa katiba ya nchi, mamlaka ya kuchagua iko mikononi mwao.

Kutoka kwenye vituo hivyo 35 vya redio, jumla ya kazi 992 (habari na vipindi) zilichunguzwa. Kwa ujumla, angalau kwenye taarifa za habari, uripoti wa vituo vya redio ulipata habari zake kutokana na jitihada zao wenyewe na kwa uchache kutokana na matukio (uripoti unaotegemea matukio). Kwa ulinganisho, hali ya mwaka huu imekuwa bora zaidi kuliko ilivyokuwa kwenye ripoti za Yearbook za tangu mwaka 2018 mpaka 2022. Uripoti unaoongozwa na vyombo vya habari kwa mwaka 2024 ulikuwa bora zaidi kwenye kipengele cha habari (37% ikilinganishwa na 28% mwaka 2019) lakini kulikuwa na udhaifu kiasi fulani kwenye vipindi (88% ikilinganishwa na 95% za mwaka 2022).

Kuhusiana na kutumia vyanzo vingi vya habari na ulinganisho wa utendaji wa redio kuanzia mwaka 2018 mpaka 2022, hali ya mwaka huu kwenye eneo hilo kwa kiasi fulani imekuwa dhaifu kwenye uripoti wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024. Matumizi ya vyanzo vingi vya habari kwenye habari yalishuka ikilinganishwa na miaka mingine yote iliyopita (42% mwaka 2024 dhidi ya zaidi ya 50% kwa miaka iliyopita). Kwenye vipindi, utendaji ulikuwa mzuri zaidi kwa mwaka 2024 kukiwa na 72% za matumizi ya vyanzo vingi vya habari ikilinganishwa na 65% kwenye miaka mingine iliyopita. Hata hivyo, utendaji wa vituo vya redio ulitofautiana; kuna vituo vichache ambavyo vilitumia idadi nzuri ya vyanzo vya habari, mfano wa vituo hivyo ni, CG FM, El-Olama FM, Highlands FM, Kasibante FM, Mashujaa FM, Mpanda FM, Pambazuko FM, Sengerema FM, Rufiji FM, SG Five FM, na Uvinza Community Radio FM.

Ingawa wagombea ndio hulengwa zaidi kwenye kampeni za uchaguzi, kwa ujumla vituo vya redio vilikuwa na habari chache kuhusu wagombea. Ni 12% tu ya kazi zote zilizochunguzwa ndizo ziliripoti kuhusu wagombea hali ambayo ni ya chini. Hata kwenye uchache huo wa habari zilizohusu wagombea, bado utendaji wa vituo vya redio katika kuwachunguza wagombea ulionekana kutafuta taarifa za jumla jumla. Taarifa pekee nzuri ni kwamba, vituo vingi zaidi vya redio viliripoti kuhusu sera na ahadi za wagombea (56% ya taarifa zilizohusu wagombea) na wakati fulani kurejelea ilani za uchaguzi za vyama (30%).

Aidha, vyombo vya Habari vilishindwa kufanya tathmini na kuripoti mafanikio na kushindwa kwa wagombea waliokuwa madarakani, kutekeleza majukumu yao. Uchunguzi kuhusu mafanikio ya wagombea uliripotiwa kwa kiwango cha chini (10%) na uchunguzi wa kina wa wagombea waliokuwa madarakani kuhusu kushindwa kutekeleza majukumu yao ni kama haukuwepo kabisa (1%). Kwa kuzingatia umuhimu mkubwa wa vyombo vya habari kwenye nyakati za uchaguzi, udhaifu huu uliojitokeza ni mkubwa mno; vyombo vya habari vinapaswa kuchunguza kwa kina mafanikio na kushindwa kwa wagombea ili kuwawezesha wapiga kura kufanya maamuzi sahihi ya uchaguzi.

Vituo vya redio havikuwa na upendeleo wa wagombea kutoka CCM wala CHADEMA. Kulikuwa na uripoti mdogo lakini wenye usawa kwa pande zote mbili. Vile vile vyama vya CUF na ACT-Wazalendo viliripotiwa, japo kwa uchache. Wagombea kutoka vyama vingine hawakuripotiwa kabisa. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa ujumuishaji wa wanawake - kama vyanzo vya habari - ikiwa ni kipengele muhimu kwenye uripoti wa vyombo vya habari haujaboreshwa. Ile hali ya kuhitaji "kuwa na angalau mwanamke mmoja kama chanzo cha habari" ilikuwa nzuri zaidi mwaka 2018 (kwa 43% ya habari za redioni) na mwaka 2022 (kwa 44% kwa habari za redioni) kuliko ilivyo sasa mwaka 2024 (kukiwa na 38% tu). Pia, kwa upande mwingine, sauti za wananchi nyakati za uchaguzi zilionekana kupewa uzito mdogo, huku habari za

vyama vya siasa, viongozi wa serikali na viongozi wa serikali za mitaa zikipewa umuhimu zaidi.

Eneo lingine ambalo utafiti huu umeliona kuwa bado lina changamoto ni kwa vituo vingi vya redio (isipokuwa vichache tu) kukwepa kutangaza mitazamo tofauti. Hata hivyo, wananchi wanapaswa kufahamishwa kuhusu mitazamo tofauti ili kuwezesha uwepo wa maoni mbalimbali.

Utofauti kati ya redio zenye leseni za mikoa/wilaya na redio za kijamii ulikuwa ndogo mno na maranyingi utofauti huo haukuonekana waziwazi. Hata hivyo kulikuwa na utofauti wa aina mbili.

- Redio za kijamii zilifanya vizuri zaidi kwenye kuripoti maudhui yaliyohusu sera za wagombea. Inavyoonekana, vituo vya redio vya jamii vinatimiza jukumu la vyombo vya habari katika kuwaelimisha wananchi kuhusu wagombea kwa njia nzuri, angalau bora kuliko vituo vingine vya redio.

- Kuna utofauti mkubwa kati ya vituo vya redio za mikoa/wilaya na redio za kijamii kwenye suala la wagombea wa vyama vya siasa. Redio za kijamii zilitoa kipaumbele kikubwa kwa CHADEMA, wakati redio zenye leseni za mikoa/wilaya ziliripoti suala hili kwa usawa.

Wadau wa vyombo vya habari wamebainisha changamoto kadhaa zilizorudisha nyuma uwezo wa vituo vya redio kuripoti vizuri kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024. Changamoto hizi zinajumuisha ukosefu wa kuaminiana baina ya wagombea na vituo vya redio, ufupi wa muda uliotolewa kwa ajili ya kampeni (siku saba tu), na changamoto za kifedha ambazo vituo vya redio vinakumbana nazo. Kwa kuongezea, baadhi ya waandishi wa habari waliweka kipaumbele kujipatia kipato kuliko kuhudumia umma. Zaidi ya hapo, mara kadhaa vituo vya redio vinavyomilikiwa na wanasiasa kutoka chama tawala au jamaa zao, vilijizuia kutangaza habari zinazowahusu wagombea kutoka vyama vya upinzani.

Ripoti hii, kwa nguvu zote, inapendekeza uwepo wa utamaduni wa mara kwa mara kwa vyombo vya habari kuwatathmini kwa kina na kwa usawa wagombea wote wanaowania nafasi za uongozi kwa kuchunguza kufanikiwa au kushindwa kwao. Pia ni muhimu kuvialika vyanzo mbalimbali vya habari ili kuja kutoa mitazamo yao kuhusu mchakato wa uchaguzi na wagombea. Jambo hili lina umuhimu wa kipekee hasa kipindi hiki wakati nchi inajiandaa kwa ajili ya uchaguzi mkuu baadaye mwaka huu.

# 1.0Utangulizi

Mwezi Novemba mwaka 2024, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliendesha uchaguzi wake wa saba wa Serikali za Mitaa uliohusisha vyama vingi vya siasa. Baada ya uliberali wa kisiasa na uanzishwaji upya wa mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa mwaka 1992, uchaguzi shindani wa kwanza uliohusisha vyama vingi vya kisiasa ulifanyika mwaka 1994 kisha kufuatiwa na ule wa mwaka 1999, 2004, 2009, 2014 na 2019. Vituo vya redio vilifanya kazi kubwa sana kwenye kila uchaguzi.

Ripoti hii imechunguza utendaji wa vituo vya redio kipindi cha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 na namna ambavyo vituo hivyo vilizingatia maslahi ya umma. Kwa maneno mengine, ripoti hii imelenga kuonesha ni kwa namna gani vituo hivyo vya redio vilisimama kwenye utamaduni wa uandishi wa habari na hivyo kuuunga mkono uripoti wa kidemokrasia unaowajibika wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Utafiti ulichunguza uripoti wa vituo 35 vya redio, zikiwamo redio zenye leseni za mikoa na wilaya, redio za kijamii na kituo cha redio chenye leseni ya kitaifa.

Ripoti hii inatumia uchambuzi wa maudhui kwa namba na takwimu ili kuchunguza uripoti wa vituo vya redio kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 kwa kutumia viashiria vya ubora kama vile muktadha wa uripoti, vyanzo vya habari, uzingatiaji wa ilani za uchaguzi za vyama, maswali yanayohusiana na maudhui yanayohusu sera za wagombea, mafanikio au kushindwa kwao huko nyuma, na mitazamo inayowaunga au kutowaunga mkono wagombea. Uchambuzi uliongezewa thamani na taarifa zilizotokana na mahojiano na washiriki muhimu katika utafiti huu wakiwamo mameneja wa vituo vya redio, mameneja wa vipindi wa redio husika, mdhibiti wa huduma za utangazaji, na mashirika ya vyombo vya habari ili kusaidia kuelewa na kuhoji mchakato wa uchujaji wa taarifa na majukumu yao kwa kipindi chote cha utafiti.

Ripoti hii imegawanyika katika sehemu tano: utangulizi, taarifa za usuli, methodolojia au mbinu za utafiti, matokeo ya utafiti (kwa takwimu/namba na kwa ubora), hitimisho na mapendekezo. Ripoti inatoa matokeo ya jumla kabla ya kuuelekeza uwasilishaji kwenye kategoria mahsusi au vituo vya redio kulingana na leseni zao. Ripoti hii pia inapatikana kupitia tovuti ya chuo UDSM-SJMC's: (https://www.udsm.ac.tz/web/index.php/schools/sjmc) ambapo inapatikana kupitia menyu ya “Yearbook on Media Quality in Tanzania”.

# 2.0Usuli - Mfumo wa Siasa wa Tanzania

Siasa nchini Tanzania hufanyika katika mfumo wa umoja, jamhuri ya kidemokrasia kwa ngazi ya urais. Tanzania ni muunganiko wa nchi huru mbili uliotokea mwaka 1964 ukiziunganisha Tanganyika (mara nyingi ikiitwa Tanzania Bara) na Zanzibar ambayo pia hutambulika kama Visiwani. Ikiwa ni nchi ya kidemokrasia, Tanzania inafuata mfumo wa vyama vingi vya siasa ambapo kunakuwa na uchaguzi kila wakati unapopaswa kuwepo.  Kifungu namba 8 (1) (a) cha Katiba kinaeleza kwamba wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi.

Kuna aina kuu mbili za uchaguzi kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Uchaguzi Mkuu na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambapo, Uchaguzi Mkuu unahusisha kuwachagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, na madiwani, uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa upande wake unajihusisha na kuwachagua viongozi kwenye ngazi za mamlaka za serikali za mitaa kwa Tanzania bara pekee (uchaguzi huu huwa haufanyiki Zanzibar). Kila aina ya uchaguzi hufanyika kila baada ya maika mitano. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inafafanua kwamba Mamkala za Serikali za Mitaa zimewekwa ili kuimarisha nguvu za wananchi kwa kuwapa fursa ya kushiriki kikamilifu katika kupanga na kutekeleza maendeleo yao.

# 3.0 Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Tanzania Bara ulifanyika tarehe 27 Novemba, 2024.

## 3.1 Kuhoji Taratibu za Usimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

Kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, watanzania watatu—Bw. Bob Chacha Wangwe, Bw. Buberwa Kaiza, na Dkt. Anenilea Nkya—ambao walijitambulisha kama 'wananchi wenye nia njema' walifungua shauri mahakamani dhidi ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
Waliiomba Mahakama Kuu ipitie uhalali wa maamuzi yaliyotolewa na mahakama ya chini (certiorary) na itoe amri ya zuio na kubatilisha Kanuni za Matangazo ya Serikali Namba 571, 572, 573, na 574 ya Julai 12, 2024. Matangazo hayo ya Serikali yalikuwa yametolewa kwa madhumuni ya kusimamia, kuratibu na kuendesha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024. Walalamikaji walisema kuwa hii ilikuwa kinyume cha sheria, ilizidi mamlaka ya waziri, inavunja kanuni za haki ya asili, ilipingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na inaonyesha upendeleo.

Zaidi ya hapo walidai kwamba, ili kukabiliana na vitendo visivyoruhusiwa kwenye chaguzi na hoja za wapiga kura, Bunge la Tanzania limetunga sheria mpya iitwayo Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi 2024 ya Taifa No. 2 2024 (The Independent National Electoral Commission Act). Sheria hii mpya imetoa nguvu na mamlaka kwa Tume Huru ya Uchaguzi kusimamia Chaguzi za Serikali za Mitaa nchini. Walalamikaji walidai kwamba uchaguzi uliopangwa kufanyika Novemba 2024, umepangwa kufanyika kinyume na sheria hii mpya ambayo imeanza kufanya kazi hata kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa baada ya sheria hiyo kutiwa saini na Rais na kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali. Sheria imeikabidhi Tume Huru ya Uchaguzi majukumu yote ya kuratibu na kusimamia chaguzi za Serikali za Mitaa badala ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.[1]

Msimamo huo pia uliungwa mkono na Baraza Kuu la Chama cha ACT-Wazalendo lililokaa tarehe 25 Agosti, 2024, ambapo lilisisitiza kwamba kuiruhusu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa isimamie Chaguzi za Serikali za Mitaa, chama tawala (CCM) na serikali vitakuwa vimeuweka uchaguzi huo kwenye hali mbaya. Tunapoelekea kwenye uchaguzi, chama tawala na serikali vimeanza mbinu zao. Wameshaanza kuzuia uhuru wa kutoa maoni na kukusanyika. Wanatishia vyama vingine vya siasa, kufanya vitendo vya ukatili na kutosikiliza maoni ya upande mwingine. Tayari tumeshafungua kesi mahakamani tukiomba mahakama itamke kuwa ni kinyume cha sheria Ofisi ya Rais-TAMISEMI kusimamia chaguzi za serikali za mitaa" Dorothy Semu, Kiongozi wa chama cha ACT Wazalendo.

Licha ya malalamiko/madai haya, Mahakama iliamua kwamba Waziri alipotoa Tangazo la Serikali alikuwa amefanya hivyo kwa mujibu wa misingi ya kisheria, Mahakama iliongeza kuwa Waziri anaendelea kuwa na mamlaka hadi pale sheria hiyo itakapobatilishwa na sheria iliyotajwa katika kifungu cha 10 (1) (c) cha Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi ya Taifa No. 2 ya 2024. Vivyo hivyo, ilikuwa ni dhamira ya Bunge kuona kwamba Tume Huru ya Uchaguzi ya Taifa ingesimamia chaguzi za serikali za mitaa baada ya sheria inayoongoza chaguzi hizo kuwa imeshatungwa. Isingekuwepo sheria hii, mfumo uliopo wa kisheria unaosimamia chaguzi za serikali[2] za mitaa ungeendelea kufanya kazi. Bila uwepo wa sheria hiyo, haiwezi kudhaniwa kuwa Tume Huru ya[3] Uchaguzi ya Taifa ina mamlaka ya kusimamia, kuratibu na kuendesha chaguzi hizo.

## 3.2 Uandikishaji wa wapiga kura

Uandikishaji wa wapiga kura ulianza siku ya Ijumaa tarehe 11 Oktoba, na kukamilika siku ya Jumapili ya tarehe 20 Oktoba, 2024—idadi kubwa ya wenye sifa za kujiandikisha walijitokeza kujiandikisha kwenye daftari la wapiga kura. Kwa mjibu wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Mohammed Mchengerwa, jumla ya watu 31,282,331 sawa na 94.83% ya watu wote waliotarajiwa kujiandikisha walikuwa wamejiandikisha kikamilifu, huku wanawake wakiwa 16,045,559 (sawa na asilimia 51.29%) na idadi ya wanaume waliojiandikisha ni 15,236,772 (sawa na 48.71%[https://www.youtube.com/watch?v=Pgmv_YDsOyw ]). Kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019, jumla ya wapiga kura 19,681,259 walikuwa wamejiandikisha— wanaume 9,529,992 na wanawake walikuwa 10,151,267[Ofisi ya rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – Taarifa ya uchaguzi wa viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa uliofanyika tarehe 24 Novemba, 2019. ]. Hata hivyo, licha ya mafanikio hayo ya serikali katika uandikishaji wa wapiga kura, paliibuka hoja kutoka upande wa vyama vya upinzani wakidai kwamba hata watoto wa chini ya umri wa miaka 18 pia walikuwa wameandikishwa kama wapiga kura. Hoja hii ilipingwa na serikali.

---

1 Visit https://x.com/JamiiForums/status/1827740701402026034 & https://www.youtube.com/watch?v=-s6V1jKEmiw
2 https://www.youtube.com/watch?v=Pgmv_YDsOyw
3 Ofisi ya rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – Taarifa ya uchaguzi wa viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ngazi ya Vijiji, Vitongoji na Mitaa uliofanyika tarehe 24 Novemba, 2019.

Nafasi tano zilikuwa zinagombewa katika uchaguzi huo: Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa, Mwenyekiti wa Kitongoji, Wajumbe wa Baraza la Kijiji na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa. Idadi ifuatayo ya wagombea walichaguliwa kugombea kwenye nafasi hizo: Wenyeviti wa Vijiji 18,340, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa 7,545, Wenyeviti wa Vitongoji 85,522, Wajumbe wa Baraza la Kijiji (wanawake na wanaume kwa pamoja) 160,371, Wajumbe wa Baraza la Kijiji (wanawake pekee) 108,166; Wajumbe wa Kamati ya Mitaa (wanawake na wanaume kwa ujumla) 18,552, na Wajumbe wa Kamati ya Mitaa (wanawake pekee) 11,762.




**Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mh. Mohammed Mchengerwa (wa pili kushoto), akizindua kampeni ya mpiga kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024, jijini Dodoma.**

## 3.3 Ilani za Uchaguzi

Kwa kawaida vyama vya siasa huwa haviandai ilani za uchaguzi kwa ajili ya Chaguzi wa Serikali za Mitaa. Huwa vinaendesha kampeni zao kwa kutumia Ilani za Uchaguzi Mkuu, kwa hali hiyo, kwa mwaka huu 2024, vingetumia ilani za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Hata hivyo, mwaka 2024, vyama viwili vya siasa—CCM na ACT-Wazalendo—viliandaa ilani zao za uchaguzi mahsusi kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Vyama vingine vilivyobaki havikuwa na ilani za uchaguzi mahsusi kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa.




**Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu (kushoto) akizindua ilani ya uchaguzi. Picha kwa hisani ya gazeti la Mwananchi.**

## 3.4 Uteuzi wa Wagombea

Katika hatua za awali suala la uteuzi wa wagombea lilifanywa na vyama vya siasa na baadae maafisa wasimamizi wa uchaguzi kutoka Ofisi ya Rais (TAMISEMI). Jedwali No. 1 hapa chini linaonesha nafasi zilizokuwa zinagombewa dhidi ya wagombea walioteuliwa kwenye nafasi hizo na nani alichaguliwa:

**Wagombea walioteuliwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024**

| | Nafasi | Idadi ya nafasi zilizogombewa | Wagombea walioteuliwa | Wagombea waliochaguliwa | Nafasi ambazo hazikujazwa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wenyeviti wa Vijiji | 12,280 | 18,340 | 12,271 | 9 |
| 2 | Wenyekiti wa Mitaa | 4,264 | 7,545 | 4,264 | 0 |
| 3 | Wenyeviti wa Vitongoji | 63,886 | 85,522 | 63,849 | 37 |
| 4 | Wajumbe wa Kamati za Mitaa | 21,320 | 18,552 / 11,762 | 21,292 | 22 |
| 5 | Wajumbe wa Baraza la Kijiji | 230,834 | 160,371 / 108,166 | 230,655 | 179 |

*Chanzo: PO-RALG (TAMISEMI)*

## 3.5 Kuenguliwa kwa wagombea

Vyama vya upinzani vililalamika kuhusu wagombea wao kuenguliwa na maafisa wasimamizi wa uchaguzi kwenye nafasi walizokuwa wanagombea. Chama cha ACT-Wazalendo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na Chama cha Wananchi (CUF) vililalamika[4] kusumbuliwa wakati wa kushughulikia rufaa[5] za wagombea wao[Tazama: https://www.youtube.com/watch?v=a7sC8hxLZTs]. Mwenyekiti wa CHADEMA Bw. Freeman Mbowe[], aliitaka Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kuwarudisha kwenye nafasi walizokuwa wanagombea wagombea wao wote waliokuwa wameenguliwa. Akizungumza na vyombo vya habari tarehe 19 Novemba, 2024, kwenye ofisi za makao makuu ya Chama hicho jijini Dar es Salaam, alitoa wito kwa TAMISEMI kuwarudisha wagombea wote waliokuwa wameenguliwa kwenye nafasi walizokuwa wamegombea. Alieleza kwamba, kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019, wagombea wa chama chake walienguliwa, na hatimaye CHADEMA ilisusia uchaguzi huo huku akidokeza kwamba kwenye uchaguzi wa mwaka 2024 hawakuwa na mpango wa kufanya hivyo.

Akitoa maoni yake kuhusu vilio vya vyama vya upinzani, Katibu Mkuu wa Chama tawala, (CCM), Dkt. Emmanuel Nchimbi, aliiomba Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kupuuza makosa madogo madogo yaliyosababisha kuenguliwa kwa wagombea wengi wa vyama vya upinzani. Akimjibu Katibu Mkuu wa CCM, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Mh. Mohamed Mchengerwa, aliongeza muda kwa vyama

4 https://www.youtube.com/watch?v=a7sC8hxLZTs
5 See: https://drive.google.com/file/d/16UlPZ_7QcKhaXOLse57FYasuF_M8lmLz/view

vya upinzani kuwasilisha rufaa zao kwenye kamati za rufaa kwa siku mbili kuanzia 13 - 15/2024. Hatimaye, wagombea 5,589 ambao awali walikuwa wameenguliwa kwenye nafasi za kugombea, walirejeshwa kwenye nafasi hizo.

## 3.6 Kampeni za Uchaguzi na Matokeo

Kampeni za uchaguzi zilifanyika kuanzia tarehe 20 mpaka 26, mwezi Novemba, 2024. Kwa ujumla, kipindi cha kampeni kilienda vizuri, huku kukiwa na matukio madogomadogo miongoni mwa vyama vya siasa. Katika kipindi hiki, kwa maeneo mbalimbali, kampeni zilionekana kuwa za amani, huku vyama vikizingatia ratiba walizokubaliana. Uchaguzi wenyewe ulifanyika tarehe 27 Novemba, 2024. Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais (TAMISEMI) wananchi 31,282,331 walijiandikisha kupiga kura, huku waliojitokeza kupiga kura walikuwa 26,963,182 ikiwa ni sawa na 86.36% ya waliojiandikisha.

**Matokeo kwa kila chama**

| Vyama vya Siasa | Wenyeviti wa Vijiji | Wenyekiti wa Mitaa | Wajumbe wa Baraza la Kijiji | Wenyeviti wa Vitongoji | Wajumbe wa Kamati za Mitaa |
|---|---|---|---|---|---|
| CCM | 12,150 (99.01%) | 4,213 (98.83%) | 229,075 (99.31%) | 62,728 (98.26%) | 21,148 (99.3%) |
| Chadema | 97 (0.79%) | 36 (0.84%) | 1,222 (0.53%) | 853 (1.34%) | 101 (0.47%) |
| ACT Wazalendo | 11 (0.09%) | 9 (0.21%) | 232 (0.1%) | 150 (0.23%) | 29 (0.14%) |
| CUF | 10 (0.08%) | 4 (0.09%) | 105 (0.05%) | 78 (0.12%) | 16 (0.08%) |
| NCCR - Mageuzi | 1 (0.01%) | 1 (0.02%) | 16 (0.01%) | 10 (0.02%) | 2 (0.01%) |
| UMD | 1 (0.01%) | 1 (0.02%) | | 2 (0.003%) | |
| ADC | 1 (0.01%) | | 1 (0.0004%) | 1 (0.002%) | 1 (0.005%) |
| CHAUMA | | 1 (0.02%) | | | |
| CCK | | | 1 (0.0004%) | | 1 (0.005%) |
| UDP | | | | 6 (0.01%) | |
| NLD | | | 1 (0.0004%) | | |
| Demokrasia Makini | | | 3 (0.001%) | | |
| **TOTAL** | 12,271 | 4,265 | 230,655 | 63,828 | 21,298 |

Aidha, vitongoji 37 havikufanya uchaguzi tarehe 27 Novemba, 2024. Kati ya hivyo, vitongoji 8 havikufanya uchaguzi kwa kuwa wagombea wake walifariki baada ya zoezi la uteuzi. Wagombea hao walitoka katika Halmashauri za wilaya za Kilwa (2), Nanyumbu (1), Itilima (1), Ikungi (1), Manyoni (1), Uyui (1) na Mbarali (1). Aidha, vitongoji 29 havikufanya uchaguzi kutokana na sababu mbalimbali. Vitongoji 12 vitarudia uchaguzi kwa kuwa matokeo ya wagombea yalifungana. Vilevile, vitongoji 9 vitarudia uchaguzi kutokana na wagombea pekee kutopata kura za kutosheleza.

6 See: https://drive.google.com/file/d/16UlPZ_7QcKhaXOLse57FYasuF_M8lmLz/view

Vyama vya siasa vilieleza kutoridhishwa kwao na namna mchakato wa uchaguzi ulivyoendeshwa na matokeo kupatikana. Kwa mfano, chama cha ACT Wazalendo kilizitaka mamlaka husika kubatilisha matokeo na kuitisha uchaguzi mpya huku kikitoa madai ya uwepo wa udanganyifu. Kiongozi wa chama hicho Bi. Dorothy Semu, alisema kwamba matokeo yaliyotangazwa hayaendani na uhalisia wa matakwa ya wananchi kujichagulia viongozi wao huku akizitaja dosari katika mchakato mzima wa uchaguzi.



**Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mstari Chamwino Dodoma tarehe 11 Oktoba, 2024, tayari kushiriki kwenye zoezi la kujiandikisha katika daftari la wapiga kura kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024.**

## 3.7 Maoni ya Wadau baada ya Uchaguzi

Wadau mbalimbali walitoa maoni yao kuhusu matokeo ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Vyama vya upinzani, CHADEMA na ACT-Wazalendo vilipinga vikali namna uchaguzi ulivyoendeshwa, vikidokeza masuala kadhaa yaliyoonekana kuufanya uchaguzi huo kutokuwa wa kidemokrasia. Miongoni mwa sababu walizozitaja ni dosari na vurugu zilizohusishwa na utekelezwaji wa sheria. Waliuita Uchaguzi huo wa Serikali za Mitaa ‘tukio la aibu’. Akionesha hisia zake kwenye ukurasa wake wa X, Mwenyekiti wa CHADEMA Bwana Freeman Mbowe aliandika: “Kwa mara nyingine tena Taifa limeshuhudia utovu wa nidhamu na vitendo vya aibu vilivyofanywa na mamlaka za serikali kwa pamoja kushirikiana kuiba bila aibu uchaguzi huo kwa manufaa ya CCM na wagombea wake, hata kwa gharama za maisha ya watanzania. Hakika, taifa letu linaomboleza tena”[7]

Vyama vingine vya upinzani havikuonesha hisia kama zilivyooneshwa na CHADEMA na ACT-Wazalendo. CCK, NRA, na NLD walionesha mtazamo kwamba[3], pamoja na upungufu uliojitokeza, kwa ujumla, uchaguzi ulikuwa huru na wa haki. Katibu Mkuu wa NLD Bwana Doyo H. Doyo alisema: “Tusitafute utetezi kwa kushindwa kwetu kwenye uchaguzi. Tulianza kushindwa pale tuliposhindwa kuweka wagombea kwenye kila nafasi, na hatuwezi kusema uchaguzi ulichezewa” (kama ilivyoelezwa hapo juu).

Washirika wa maendeleo wakiwakilishwa na Balozi za Ireland, Norway na Sweden walielezea wasiwasi juu ya maendeleo wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Wakionyesha hisia zao wakati wa maadhimisho ya Siku

7 Visit the following link for the clip covering NLD press conference posted at Wasafi FM instagram page: https://www.instagram.com/wasafifm/reel/DDCKFOjsLcP/

ya Haki za Binadamu duniani yaliyofanyika tarehe 10 Desemba, 2024, Balozi wa Sweden alisema: “ Hata hivyo, tuna wasiwasi kuhusu ripoti za kuaminika za hivi karibuni, kabla na wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa, kuhusu dosari za uchaguzi, kutoweka kwa watu na vurugu dhidi ya raia na wanasiasa hai. Tunaunga mkono madai ya kufanyika kwa uchunguzi wa wazi na huru kuhusu madai haya. Na bado tuna matumaini kwamba kuzishughulikia changamoto zilizopo[8] kutatengeneza jukwaa muhimu kuwezesha uchaguzi wa amani, huru na wa haki mwaka 2025,”-Balozi Charlotta Ozaki Macias.


Akiwahutubia wajumbe wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Jaji Mstaafu, Joseph S. Warioba alisisitiza kwamba yaliyojiri kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yametengeneza tishio kubwa kwa amani ya nchi. Alidokeza kwamba wananchi walijaa matumaini kwamba Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 ungekuwa tofauti na ule wa mwaka 2019. Akitoa maoni yake kuhusu kuenguliwa kwa wagombea wengi wa upinzani kwa hoja kwamba walijaza vibaya fomu za kuomba kuteuliwa, Jaji huyo mstaafu alidokeza: “Ni ngumu kwa umma kuamini kwamba walioenguliwa walifanya makosa hayo kwani wote walioenguliwa walitoka upande mmoja. Vipo vyama ambavyo wagombea wao wanazijua na kuzifuata kanuni, na kuna vyama ambavyo wagombea wao hawako hivyo. Alionya kwamba, labda mambo yabadilike hapa katikati, vinginevyo Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 utazungukwa na changamoto zile zile. “Pamoja na majadiliano ya tangu 2019 mpaka sasa, mambo yaliyouzunguka uchaguzi wa mwaka huu hayana tofauti yoyote na yale yaliyotokea mwaka 2019. Kwa hiyo, uchaguzi mkuu wa mwakani, 2025, utakuwa na mambo yale yale,[9] labda kama patachukuliwa hatua madhubuti za kuepukana nayo”

## 3.8 Uhuru wa Vyombo vya Habari kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024

Uhuru wa vyombo vya habari ni moja ya mihimili ya demokrasia na uchaguzi. Ikiwa uhuru huo utatishiwa, basi deomokrasia na uchaguzi vyote vitakuwa matatani. Uhuru wa vyombo vya habari ni muhimu kwa demokrasia, na uchaguzi wa kidemokrasia hautaweza kufanyika pasipo uhuru wa vyombo vya habari. Uchaguzi huru na wa haki hauhusiani na uhuru wa kupiga kura tu bali pia unahusiana na ufahamu wa jinsi ya kupiga kura na ufahamu wa ushirikishwaji ambapo wapiga kura hushiriki katika majadiliano na kuwa na taarifa zote muhimu kuhusu vyama vya siasa, sera zao, wagombea wao, na mchakato mzima wa uchaguzi ili kuwawezesha wapiga kura kufanya maamuzi sahihi.

Tofauti na mazingira ya vyombo vya habari yalivyokuwa wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019, ambapo kwa uwazi kabisa palikuwa na mazingira ya udhibiti, mazingira ya uhuru wa vyombo vya habari kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024, yalionekana kuimarika. Mazingira ya uhuru wa vyombo vya habari yalianza kuimarika tangu mwaka 2022 baada ya kuanguka ghafla kati ya mwaka 2016 na 2021. Ripoti ya mwaka 2024 ya Waandishi wa Habari Wasio na Mipaka ijulikanayo kama ‘Reporters without Borders’ Press Freedom Index’ imeiweka Tanzania katika nafasi ya 97 kati ya nchi 182 duniani kuhusu kuheshimu uhuru wa vyombo vya habari. Jedwali lifuatalo linaonesha nafasi ya Tanzania tangu mwaka 2016 hadi 2024:

**Hali ya Uhuru wa Habari Tanzania 2016-2024**





Kwenye upande chanya wa mazingira ya vyombo vya habari, ripoti ya Hali ya Vyombo vya Habari Nchini Tanzania (2022-2023) iliyotolewa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) inasomeka hivi: “Utafiti umebaini kwamba tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani mwezi Machi mwaka, 2021, alifuata mkondo wa kimaendeleo kuhusiana na uhuru wa vyombo vya habari na utendaji wake nchini Tanzania ikilinganishwa na kipindi kilichotangulia kabla yake. Maneno na matendo yake kipindi chote cha utafiti huu yametengeneza mazingira rafiki, yanayoviwezesha vyombo vya habari na wanahabari kutekeleza majukumu ya taaluma yao kwa uhuru zaidi” (MCT, 2024:8). Hata hivyo, ripoti inabainisha kwamba, licha ya kuboreshwa kwa mazingira, sheria zinazokandamiza uhuru wa kujieleza bado zimo kwenye vitabu vya sheria.

Zaidi ya hapo, kwenye utafiti wake, Afrobarometer iliwataka washiriki wake barani Afrika kutoa maoni yao kwenye swali lifuatalo: “Ni kwa namna gani kwenye nchi hii vyombo vya habari vina uhuru wa kuripoti na kutoa maoni kuhusu habari bila udhibiti au kuingiliwa na serikali?” matokeo ya utafiti yanaonesha Tanzania iko nafasi ya kwanza kati ya nchi 39 barani Afrika.

8 See: https://thechanzo.com/2024/12/11/tanzanias-key-development-partners-concerned-about-reports-of-irregularities-disappearances-and-violence-before-and-during-local-elections/
9 https://ippmedia.com/the-guardian/news/local-news/read/national-unity-now-in-peril-cautions-warioba-2024-12-04-192844

**Figure 12: How free is the media?** | 39 countries | 2021/2023




***Respondents were asked:*** *In your opinion, how free is the news media in this country to report and comment on the news without censorship or interference by the government?*

Hata hivyo, tafiti zingine zinatuonesha picha tofauti kabisa kuhusiana na uhuru wa kujieleza nchini. Ripoti ya The Freedom in the World ya mwaka 2024 iliyotolewa na The Freedom House imeiweka Tanzania namba 1 kati ya alama 4 kwenye swali linalouliza, "Je kuna uhuru na kutoingiliwa kwa vyombo vya habari?"

Kwenye utafiti wa Twaweza uliowashirikisha waandishi wa habari 1,202 uliokuwa na kichwa cha habari, "Sauti za Waandishi" nusu ya waandishi walioshiriki utafiti huo walibainisha kwamba walikuwa wakitishiwa, kunyanyaswa au kushambuliwa (Twaweza, 2024:2) huku vyanzo vikubwa vya vitisho hivyo vikiwa ni kutoka kwa maafisa wa serikali.

## 3.9 Dhima ya Vyombo vya Habari kwenye Uchaguzi

Kwenye uchaguzi, vyombo vya habari vina dhima mbili. Seti ya kwanza inatokana na suala la mtazamo wa kiweledi ikiwa limejikita kwenye kuwajibika kwa jamii na dhima ya pili ni ya wajibu wa vyombo vya habari kisheria. Kwa ujumla, vyombo vya habari vina jukumu lao katika kutoa taarifa, kuelimisha na hatimaye kuwawezesha wananchi kwa kutoa taarifa sahihi, na kwa wakati, kwa kuzingatia muktadha, zinazofaa, na zilizofanyiwa utafiti kuhusu mchakato mzima wa uchaguzi. Jukumu hilo hujumuisha kuwakusanya wananchi pamoja ili kuchukua hatua na kushiriki katika uchaguzi. Kwa hivyo, vyombo vya habari ni mdau muhimu na asiyefaa kuepukwa ili kuwa na uchaguzi huru na wa haki.  Zaidi ya hayo, vyombo vya habari vina jukumu la kijamii na jukumu la kitaaluma. Kwa mtazamo wa kitaalamu, vyombo vya habari vina majukumu matatu muhimu.

- **Vyombo vya habari kama muelimishaji jamii:** Vyombo vya habari vinaelimisha wananchi kuhusu mchakato wa uchaguzi, na hutoa taarifa ili kuwawezesha wapiga kura kufanya maamuzi sahihi (kupiga kura kwa busara).

- **Vyombo vya Habari kama Jukwaa la Kampeni na Uwanja wa Majadiliano:** Vyombo vya habari hutumika kama jukwaa la majadiliano kuhusu maoni na mawazo kinzani baina ya wagombea na wapiga kura.

- **Vyombo vya habari kama mlinzi muangalizi:** Vyombo vya habari hufanya kazi kama mlinzi, vikitia jicho lake pale ambapo panaweza kuharibu mchakato wa uchaguzi, na hivyo kuhakikisha panakuwa na uchaguzi wa haki na huru.

Usimamizi wa uchaguzi nchini unaongozwa na taratibu maalumu za kisheria zinazojumuisha wadau wote vikiwamo vyombo vya habari. Taratibu hizi za kisheria zinavitaka vyombo vya habari kuhakikisha vinafanya uripoti wa masuala ya uchaguzi kwa usahihi, usawa na kuzingatia ulinganifu kwa vyama vya siasa na wagombea. Hivyo, wajibu huu wa kisheria unaunda seti ya pili ya dhima za vyombo vya habari nyakati za chaguzi nchini.

## 3.10 Methodolojia na Mbinu za Utafiti

Utafiti huu umechunguza uripoti wa Uchaguzi za Serikali za Mitaa kwa kuangazia uchambuzi wa maudhui ya kazi za kihabari na mahojiano yaliyofanyika kwa mameneja wa vituo na mameneja wa vipindi wa vituo vya redio. Jumla ya vituo vya redio thelathini na vitano (35) vilichaguliwa kwa ajili ya kufanyiwa utafiti.[10]

### 3.10.1 Mtazamo wa Jumla kuhusu Uripoti wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Kuzingatia Viashiria vya Ubora

Aina mbili za vigezo vya ubora[Mbinu kamili za kiutafiti zilizotumika kwenye utafiti huu zimeambatanishwa mwishoni mwa ripoti hii. ] vilitumika kwenye uchambuzi wa maudhui - viashiria vya ubora vinavyohusiana na uchaguzi wenyewe na viashiria vya ubora vinavyohusiana na uandishi wa habari. Vigezo vya ubora vinavyohusiana na uchaguzi wenyewe vinajumuisha uzingatiaji wa ilani za uchaguzi za vyama, maudhui dhidi ya haiba ya mtu, uchunguzi wa kina wa mafanikio ya wagombea, uripoti wa wagombea na vyama vya siasa, n.k. Vigezo vya ubora vinavyohusiana na uandishi wa habari vinajumuisha muktadha wa uripoti, vyanzo vya habari, maadili n.k. Utafiti wa Yearbook kuhusu ubora wa uripoti unatumia neno "ubora" kama dhana inayoonesha muhtasari wa jumla ya vigezo mbalimbali ambavyo kimsingi vinapaswa kuzingatiwa katika uripoti kwa sababu ubora ukichukuliwa kama kitu "kimoja" ni ngumu kufikiwa. Badala yake, vikitumika vigezo mbalimbali mahsusi, itakuwa rahisi kupima ubora kama namna jumuishi ya kupima kiwango cha namna vyombo vya habari vinavyofanya kazi. Vigezo vya ubora vilivyotumika kwenye utafiti wa Yearbook wa mwaka 2024 vimeandaliwa kulingana na nadharia ya uandishi wa habari, utendaji wa tasnia hii na tafiti zilizohusu uripoti wa vyombo vya habari kuhusu chaguzi. Vifuatavyo ni vigezo vya ubora vilivyotumika kwenye utafiti huu:

10 A complete methodological approach is attached at the end of this report.

- **Muktadha wa Uripoti:** Kigezo hiki kinachunguza matukio na matamko ambayo yalileteleza uripoti wa uchaguzi. Pia kinachunguza ikiwa waandishi wa habari wanaripoti matukio au wanakusanya habari zao wenyewe za uchaguzi. Uchambuzi huu una malengo mawili: mosi, kuangalia mtawanyiko wa uripoti miongoni mwa vyama vya siasa, na pili, kulinganisha uwiano wa uripoti baina ya habari zinazotokana na matukio na habari ambazo zinaandikwa kwa jitihada binafsi za chombo cha habari.

- **Vyanzo vya habari:** Hapa tunaangalia angalau uwepo wa vyanzo viwili vya habari kwenye kila kazi ya kihabari. Iwe habari au kipindi, jambo hili lina umuhimu mkubwa katika uripoti wa uchaguzi. Utaratibu huu unawawezesha waandishi wa habari kuja na mitazamo mbalimbali kwenye kazi zao na hivyo kuwa na taarifa za kina ambazo huwasaidia wapiga kura kufanya maamuzi sahihi. Zaidi ya hapo inatuhakikishia kuwa sauti za wadau mbalimbali zinasikika, zikiwamo sauti za wananchi wa kawaida—ambao mara nyingi huwa wanasahaulika.

- **Mawanda tofauti ya Uripoti wa Wagombea:** Kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, tulitahmini uwakilishi wa wagombea kwa kuzingatia nafasi walizokuwa wanagombea: mwenyekiti wa kijiji, mwenyekiti wa kitongoji, wajumbe wa kamati za mitaa, wajumbe wa mabaraza ya vijiji, wajumbe wanawake kwenye kamati za mitaa, na wajumbe wanawake kwenye mabaraza ya vijiji. Lengo la kufanya hivi lilikuwa ni kubainisha kama kulikuwa na ulinganifu au upendeleo katika uwakilishi kwa nafasi zote ambazo ziligombewa.

- **Mawanda tofauti ya mada zilizoripotiwa:** Kigezo hiki kilichunguza mada zilizohusiana na uchaguzi na masuala mengine yaliyoripotiwa kwenye kazi za kihabari kama vile habari au vipindi. Lengo ni kutengeneza picha ya vyombo vya habari kulingana na mwelekeo wa uripoti wao, ama wamezingatia siasa, maendeleo, uchumi, na masuala mengine muhimu.

- **Uripoti wa maudhui kuhusu sera (mpya):** Vyombo vya habari vina dhima kubwa ya kuwaelimisha wananchi kuhusu sera za wagombea na maono yao ya siku za usoni. Uandishi wa habari bora zaidi lazima uweke kipaumbele kwenye uchambuzi mpana na wa kina kuhusu sera hizi, uchambuzi ambao utawawezesha wapiga kura kufanya maamuzi sahihi. Kwa kumakinikia zaidi kwenye ahadi za wagombea, vyombo vya habari vinaweza kutoa muktadha, kubainisha matokeo ya muktadha huo, na kujadili namna sera hizi zinavyoendana na tunu na mahitaji ya jamii. Lengo ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata taarifa sahihi na za kina kuhusu wagombea na hivyo kuonesha nafasi yao katika kuongeza uwajibikaji na ushiriki wao kwenye mchakato wa kidemokrasia.

- **Kurejelea kwenye ilani ya chama:** Kurejelea kwenye ilani ya chama cha mgombea ni muhimu mno kwenye uripoti wa uchaguzi kwa sababu nyaraka hizi zinadokeza sera na programu ambazo kila mgombea anaziunga mkono. Kwa kuzichambua na kuzijadili kwa kina ilani hizi za uchaguzi, waandishi wa habari watakuwa wamewapa wapiga kura ufahamu mpana wa kila mgombea na sera zake na namna ahadi zao zinavyolenga kutatua changamoto mahsusi katika jamii. Uripoti huu wa kina huwawezesha wapiga kura kufanya maamuzi sahihi na kuwawajibisha wagombea kulingana na ahadi zao. Ni muhimu kwa waandishi wa habari kuzielewa na kuzifikisha taarifa hizi kwa wapiga kura ili kuhakikisha kuwa wapiga kura wana taarifa zote za msingi wakati wa mchakato wa uchaguzi.

- **Kufanikiwa na Kushindwa:** Waandishi wa habari wanaoripoti kuhusu wagombea nyakati za uchaguzi, wanapaswa wasiripoti mafanikio ya wagombea pekee, bali pia waripoti kuhusu kushindwa kwao ili kuwapa wananchi picha kamili ya mgombea fulani.

- **Uwepo wa Mitazamo:** Wakati vikitafuta vyanzo vyao vya habari, vyombo vya habari vinapaswa kutoa nafasi sawa kwa vyanzo vya habari vyenye mitazamo tofauti inayowahusu wagombea ama kuwaunga mkono au kinyume chake. Jambo hili ni muhimu mno kwani linawajengea uwezo wapiga kura kuwaelewa wagombea na vyama vyao na hatimaye kupiga kura kwa usahihi.

- **Kuuliza Maswali wakati wa Mahojiano:** Wakati wa mahojiano, wandishi wa habari wanatarajiwa kuuliza maswali kuhusu kauli za wagombea. Hii itawasaidia wasikilizaji kupata uelewa wa kina kuhusu sera za wagombea.

Uripoti wa uchaguzi kwa kuzingatia vigezo vya ubora vilivyobainishwa ni suala la msingi mno hasa nyakati hizi ambapo uandishi wa habari wa kiraia umeshika kasi. Uwepo wa majukwaa mbalimbali ya vyombo vya habari unaruhusu watu kubadilishana mitazamo na taarifa, vile vile inaonesha umuhimu wa kuzingatia vigezo vya kitaaluma vya uandishi wa habari. Vyombo vya habari na waandishi wa habari wanawajibika kuhakisha wanazingatia ubora katika uripoti wao ili kuwajengea ufahamu wananchi. Kuwa na watu wenye taarifa sahihi ni muhimu ili kuwawezesha wapiga kura kufanya uchaguzi unaoakisi tunu na maslahi yao wakati wa uchaguzi.

Uripoti bora una dhima muhimu katika kutofautisha uandishi wa habari wa kiraia dhidi ya ule wa asili. Wakati uandishi wa habari wa kiraia unaweza kukupa ufahamu muhimu na mitazamo ya msingi tu, waandishi wa habari walioiva kitaaluma wana jukumu la kuchimba zaidi na kufunua ukweli usiojulikana kuhusu matukio na masuala ambayo kwa kiasi kikubwa huipa jamii mwelekeo wakati wa mchakato wa uchaguzi. Aina hii ya uandishi inaweza kuchukua sura nyingi, ikiwa ni pamoja na uripoti wa ufafanuzi ambao unataka kuujulisha umma kuhusu ukweli wa jambo fulani au uandishi wa habari wa ufafanuzi ambao una lengo la kufafanua masuala magumu na hatimaye kuwasaidia wapiga kura kuelewa matokeo ya maamuzi yao. Kimsingi ubora wa uripoti wa uchaguzi ni msingi wa demokrasia, kwani huwawezesha wapigakura kuwa na uelewa muhimu kwa ajili ya kushiriki kikamilifu kwenye mchakato wa uchaguzi.

### 3.10.2 Sampuli ya Vituo vya Redio

Ili kutafiti ubora wa uripoti kwenye taarifa zao za habari na vipindi, utafiti huu umechunguza vituo 35 vya redio na kituo kimoja cha utangazaji cha kitaifa. Awali tulichagua vituo 40 vya redio kuwa kwenye sampuli yetu; hata hivyo, vituo vitano havikuweza kukidhi vigezo vilivyohitajika kwa ajili ya utafiti huu. Hili lilisababishwa na mambo kadhaa ikiwamo matatizo ya muda mrefu ya kiufundi yaliyokuwa yakiharibu taratibu za matangazo yao. Matokeo yake, mara nyingi wakati wa kurekodi vipindi kwa ajili ya utafiti huu, vituo hivi havikuwa hewani na hivyo kuwa vigumu kupata idadi iliyohitajika ya vipindi kwa ajili utafiti. Kwa hiyo, utafiti huu ukajielekeza zaidi kwenye vituo 35 vilivyokuwa vimebaki ambavyo vilionekana kuwa na uthabiti endelevu na wa uhakika ili kupata taarifa zao za habari na vipindi. Jedwali lifuatalo linaonesha vituo vilivyotumika kama sampuli ya utafiti huu kwa kuzingatia kanda viliko:


**Sampuli ya vituo vya redio** — 35 Vituo vya redio vilivyofanyiwa utafiti

| Kanda | Vituo vya redio | | |
|---|---|---|---|
| 01 Kanda ya Mashariki | TBC Taifa, Chalinze FM, Jamii FM | Mashujaa FM, Pambazuko FM, Pangani FM | Rufiji FM, TK FM |
| 02 Kana ya Kaskazini | Arusha One FM, Manyara FM | Sunrise FM, Moshi FM | |
| 03 Kanda ya ziwa | Bariadi FM, Bunda FM | Kasibante FM, Kwizera FM | Sengerema FM, Flamingo FM |
| 04 Kanda ya kati | CG FM, Dodoma FM, Standard Radio | Uvinza Community FM, Uyui FM | KICORA FM, SG FIVE FM |
| 05 Nyanda za juu kusini | Highlands FM, Ileje FM, Mbeya City FM, Mpanda FM | Ruvuma FM, VOS FM, El-Olama FM | Nuru FM, Pamoja FM, Vwawa FM |

Tukiiweka pembeni TBC Taifa, ambayo ni kituo cha utangazaji cha umma chenye leseni ya kitaifa, vituo vyote vilivyobaki vinafanya kazi kwa aina mbalimbali za leseni zikiwemo leseni za wilaya, mkoa na za kijamii. Utofauti huu kwenye sampuli ni muhimu sana kuwepo ili kuweza kuonesha utofauti wa mawanda ya utangazaji na masafa miongoni mwa vituo vilivyo kwenye sampuli ya utafiti. Kwa muundo wa umiliki, sampuli hii imeundwa na vituo vya redio vinavyomilikiwa na taasisi binafsi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na redio zinazomilikiwa na jamii. Ujumuishaji wa sampuli kwa mtawanyiko huo ni muhimu mno na ulifanywa kwa kukusudia. Kuwa na vituo vyenye utofauti wa namna hii ya umiliki kwenye sampuli kunatupa ufahamu mzuri wa kuijua tasnia ya redio za ndani ilivyo nchini, tutaweza kujua upekee wa mitazamo mbalimbali ya vituo vya redio, mpangilio wao wa vipindi, na jitihada za ushirikishaji wa wanajamii nchini kote. Mtindo huu wa kupata sampuli una manufaa makubwa kwenye utafiti na unaonyesha umuhimu wa redio za ndani kama nyenzo ya kukuza uhusiano na sauti za jamii ya ndani.

### 3.10.3 Sampuli ya Kazi za Kihabari

Licha ya kuwa na sampuli ya redio za ndani, pia kulikuwa na sampuli ya kazi za kihabari (taarifa za habari na vipindi) ambavyo vilikusanywa kwa siku 16 ndani ya wiki tatu kuanzia tarehe 11 Novemba, 2024 mpaka 01 Desemba, 2024 kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapa chini:




Kwa ujumla, kazi za redioni (habari 686 na vipindi 306) zilikusanywa kutoka vituo 35 vya redio. Kwa kuzingatia kwamba utafiti huu ulihusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kazi zilizokusanywa kwenye sampuli ni zile ambazo zilihusiana na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa tu ambazo jumla yake ilikuwa 992, na ndizo zilizotumika kama kiunzi cha mwisho cha uchambuzi.

### 3.10.4 Mafunzo kwa Waandishi na Wasimbaji

Mradi uliendesha mafunzo kumbushi ili kuimarisha ujuzi kwa waandishi na wasimbaji ambao wamekuwepo kwa muda pamoja na wapya. Mafunzo ya kina kwa waandishi (Transcribers) yalifanyika kwa siku moja, na yaliangazia zaidi mbinu za kuwezesha kuzitafsiri sauti kwenda kwenye maandishi kwa usahihi na umahiri. Wakati huo huo, wasimbaji walishiriki kwenye mafunzo ya kina ya siku nne yaliyoangazia zaidi kwenye kitabu cha misimbo, mbinu za usimbaji na namna bora ya kusimba. Kwa ufanisi mkubwa mafunzo hayo yalijumuisha washiriki 18, jumla ambayo iliwajumuisha waandishi na wasimbaji kwa pamoja. Ikiwa sehemu ya utamaduni wa mradi, vipindi vyote vilivyorekodiwa vilifasiriwa kwenda kwenye maandishi ambayo yalitumiwa kama kitendea kazi muhimu kwa wasimbaji. Utaratibu huu uliwawezesha wasimbaji kufanya kazi kwa kutumia maandishi yaliyofasiriwa kutoka kwenye kazi zilizorekodiwa redioni kuliko kama wangetumia sauti kama zilivyorekodiwa kutoka redioni, na kwa hiyo iliwezesha mchakato wa usimbaji kuwa shughulishi na fanisi. Kwa kusimba programu ambazo tayari zilikuwa zimeshawekwa kwenye maandishi, wasimbaji walikuwa wakijishughulisha zaidi na maudhui yaliyopangiliwa vizuri.

### 3.10.5 Udhibiti ubora wa kazi zilizokuwa zimerekodiwa na usimbaji

Udhibiti ubora ni kipengele muhimu kwenye mradi wa Yearbook, jambo hili linatumika kama kiunzi muhimu cha kuzifanya data zinazochambuliwa zibaki kuwa sahihi na zenye kuaminika. Mchakato wa udhibiti ubora ulijumuisha hatua mahsusi za kuthibitisha na kujiridhisha kwamba kila kipindi cha redio kilichorekodiwa kilikuwa kimerekodiwa kikamilifu na kiko tayari kwa ajili ya kuandikwa kwa maneno. Kwenye kila mchakato wa kurekodi kipindi palihakikishwa panafanyika utaratibu mzuri na kujiridhisha kwamba hakuna kitu chochote kinachokosekana na kwamba kila sauti inayorekodiwa inasikika vizuri na kwa ubora unaotakiwa. Zaidi ya hayo, maandishi yaliyoandikwa kutokana na vipindi yalihifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya baadae yatakapohitajika. Zoezi la kuhifadhi kazi hizo lilikuwa na umuhimu mkubwa kwani lilisaidia kuondoa utata pale ambapo ulijitokeza wakati wa uchambuzi wa data. Taarifa zilizokuwa zimewekwa kwenye maandishi zilithibitisha kuwa na umuhimu mkubwa hasa pale ulipokuwa unatolewa ufafanuzi kuhusu masuala ya usimbaji na hivyo kujihakikishia kuwa uchambuzi wetu ulikuwa wa uhakika na wenye data za kuaminika. Kwa kuvitimiza vigezo vya udhibiti ubora, tulilenga kutimiza kikamilifu viwango vya hali ya juu vya ubora wa utafiti.

# 4.0 MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya utafiti huu. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa mtindo wa ngazi ambapo, ngazi ya-1 inahusu matokeo ya jumla ya vituo vyote vya redio, ngazi ya pili-2 ni matokeo yanayohusu vituo vya redio vyenye leseni za mikoa na wilaya na matokeo yake yalilinganishwa na yale ya redio zenye leseni za kijamii, na ngazi ya-3 ni matokeo ya kituo cha utangazaji chenye leseni ya taifa-TBC Taifa. Kwa mwaka 2024 sampuli ilikuwa na kazi 992 zilizorekodiwa kutoka vituo 35 vya redio.


### 4.1.1 NGAZI YA 1: Uchambuzi wa jumla kwa vituo vyote vya redio

### 4.1.2 Aina ya kazi

Kati ya kazi 992 zilizochambuliwa, 686 (69%) zilikuwa habari na 306 (31%) vilikuwa ni vipindi vya redio.

### 4.1.3 Aina

Aina ya kazi ndio hubainisha maudhui ya vipindi vya redio. Utafiti huu umebaini kwamba 70% ya kazi zote zilikuwa ni habari, 15% ni makala, mijadala ilikuwa (4%) na mahojiano (8%) kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:




Jedwali hapo juu linaonesha ni kwa namna gani vituo tofauti vya redio vilitumia aina tofauti za kazi. Vipo vilivyofanya vizuri kwenye makala na vingine kwenye majadiliano na mahojiano, Hata zile redio ndogo kabisa ziliweza kutoa kazi za aina mbalimbali. Manyara FM, Pangani FM, SG FM, na Kasibante FM zilikuwa ni redio ambazo zilitenga muda kuwaelimisha wananchi kupitia vipindi vya makala, mijadala na mahojiano. Kwa mfano, 13% ya vipindi vya Manyara FM vilikuwa ni majadiliano na 19% ni mahojiano. Kasibante FM, 25% ya vipindi vyake vilikuwa ni makala, 13% majadiliano, ilihali 13% nyingine ilikuwa ni mahojiano. Pangani FM ilikuwa na 16% ya vipindi vya makala, huku majadiliano yakipewa asilimia 11% ya vipindi vyote na mahojiano yalikuwa 32%. SG FM ilikuwa na 23% ya vipindi vya makala, majadiliano yalikuwa 15% na 15% ni mahojiano.

| Aina kwa mujibu wa vituo vya redio (idadi iliyojuu ya wastani imewekwa kwenye rangi maalumu) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Vituo vya redio | Habari | Makala | Majadiliano | Mahojiano | Visivyotambulika |
| Wastani | 70% | 15% | 4% | 8% | 2% |
| Arusha One FM | 58% | 29% | 0% | 4% | 8% |
| Bariadi FM | 71% | 19% | 0% | 5% | 5% |
| Bunda FM | 76% | 12% | 3% | 6% | 3% |
| CG FM | 67% | 30% | 0% | 3% | 0% |
| Chalinze FM | 65% | 19% | 0% | 12% | 4% |
| Dodoma FM | 80% | 8% | 5% | 8% | 0% |
| El-Olama FM | 54% | 21% | 13% | 8% | 4% |
| Flamingo FM | 90% | 6% | 0% | 4% | 0% |
| Manyara FM | 56% | 0% | 13% | 19% | 13% |
| Highlands FM | 64% | 11% | 4% | 14% | 7% |
| Ileje FM | 72% | 11% | 6% | 6% | 6% |
| Jamii FM | 69% | 22% | 0% | 6% | 3% |
| Kasibante FM | 44% | 25% | 13% | 13% | 6% |
| KICORA FM | 81% | 3% | 10% | 7% | 0% |
| Sunrise FM | 69% | 19% | 13% | 0% | 0% |
| Mashujaa FM | 64% | 21% | 0% | 0% | 14% |
| Mbeya City FM | 62% | 29% | 0% | 10% | 0% |
| Moshi FM | 68% | 16% | 11% | 5% | 0% |
| Mpanda FM | 62% | 27% | 12% | 0% | 0% |
| Nuru FM | 79% | 7% | 2% | 10% | 2% |
| Pambazuko FM | 56% | 15% | 7% | 15% | 7% |
| Pamoja FM | 63% | 25% | 3% | 9% | 0% |
| Pangani FM | 42% | 16% | 11% | 32% | 0% |
| Kwizera FM | 82% | 6% | 6% | 6% | 0% |
| Sengerema FM | 72% | 6% | 0% | 22% | 0% |
| Rufiji FM | 45% | 25% | 15% | 10% | 5% |
| Ruvuma FM | 76% | 19% | 0% | 5% | 0% |
| SG FIVE FM | 46% | 23% | 15% | 15% | 0% |
| Standard FM | 88% | 4% | 0% | 8% | 0% |
| TBC Taifa | 82% | 18% | 0% | 0% | 0% |
| TK FM | 74% | 12% | 5% | 2% | 7% |
| Uvinza Community FM | 44% | 38% | 0% | 19% | 0% |
| Uyui FM | 68% | 3% | 7% | 23% | 0% |
| VOS FM | 69% | 17% | 6% | 6% | 3% |
| Vwawa FM | 100% | 0% | 0% | 0% | 0% |


### 4.1.4 Muktadha wa uripoti

Sababu ya kuuzingatia muktadha wa uripoti ni kubainisha kama vituo vya redio vinaandaa kazi zao kwa kuzingatia matukio au kwa jitihada zao wenyewe. Pamoja na kwamba matukio ni muhimu, vyombo vya habari vinapaswa kutafuta habari zao wenyewe na kutengeneza ajenda ili kuhimili ushindani na kuwa mbele ya vyombo vingine vya habari. Mwaka 2024, matukio yamechangia asilimia 63.2% ya kazi kwenye kipengele cha habari, na asilimia 36.8% tu ndio ilitokana na jitihada binafsi za vyombo vya habari. Kinyume chake, kwenye, vipindi, asilimia 12.4% tu ndio zilitokana na matukio wakati asilimia 87.6% ilitokana na jitihada binafsi za vyombo vya habari.




Ukilinganisha hali hii na ile iliyojitokeza tangu mwaka 2018 mpaka 2022, utaona kwa uwazi kabisa kwamba uripoti uliotokana na jitihada binafsi za vyombo vya habari kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa umeimarika zaidi kwenye kipengele cha habari kwa asilimia 36.8% ikilinganishwa na asilimia 28% mwaka 2019, lakini kwenye vipindi kumekuwa dhaifu kidogo (88% ikilinganishwa na 95% mwaka 2022). Hali hii inatoa dokezo la ukweli kwamba vituo vya redio bado vinakosa msukumo na rasilimali fedha ili kuripoti habari zao wenyewe.

## Muktadha wa upatikanaji habari kwa vituo vya redio




*Chanzo: Yearbook on Media Quality in Tanzania 2018, 2019 and 2022*


### 4.1.5 Uripoti kwa mada

Utafiti huu ulichunguza uripoti kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024. Kwa sehemu kubwa vyombo vya habari viliripoti zaidi mada ya uchaguzi kuliko mada nyingine. . Mada nyingine ambazo ziliguswa kwa uchache zilikuwa ni pamoja na masuala ya usalama wa taifa, masuala ya kisheria, rushwa, uharifu, na magonjwa. Kwa ujumla wake, kazi zilizohusu mada hizi zilikuwa chini ya 3% ya kazi zote.

### 4.1.6 Vyanzo vya Habari


Vyanzo vya habari ni muhimu kwa sababu hutoa ufahamu tofauti, muegemeo na kazi bora za kihabari. Vyombo vya habari kutumia vyanzo vingi vya habari (vyanzo 2 au zaidi) kwenye habari ilikuwa ni 42.2% kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na zaidi ya 50% kwenye tafiti zilizotangulia za mwaka 2018-2022. Hata hivyo, kwenye vipindi, imekuwa kinyume chake. Hali iliyojitokeza kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024 ilikuwa bora zaidi, kwa 71.8% kwenye kutumia vyanzo vingi vya habari ikilinganishwa na karibu 65% mwaka 2018-2022. Jedwali lifuatalo linatoa taarifa zaidi.

## Vyanzo vya habari





Kwa miaka minne iliyopita, tumewafundisha waandishi wa habari jinsi ya kuripoti habari zao na kutafuta vyanzo vya habari vyenye maoni na mitazamo tofauti. Pamoja na hayo, bado tumeona habari zenye chanzo kimoja tu cha habari. Baadhi ya vituo vya redio vimefanya vizuri kwenye kipengele hiki cha kutumia vyanzo vingi vya habari kwenye uripoti wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024. Wakati wa uripoti wa Uchaguzi huo wa Mwaka 2024, baadhi ya vituo vya redio vilivyojaribu kutafuta vyanzo vingi vya habari (vinne na zaidi) ni: CG FM (76%), El-Olama FM (46%), Kasibante FM (31%), Mpanda FM (44%), Pambazuko FM (52%), Sengerema FM (36%), Rufiji FM (30%), na Uvinza Community FM (56%). Jedwali lifuatalo linabainisha asilimia ya vyanzo vya habari vilivyotumika kwa kila kituo cha redio kilichojumuishwa kwenye utafiti huu.

# Idadi ya vyanzo vya habari kwa kituo cha redio



Kwenye uandishi wa habari, vyanzo vya habari ni muhimu kwa sababu huwapatia waandishi wa habari ufahamu, muegemeo tofauti na hivyo kuwa na kazi bora za kihabari kuliko ikifanyika vinginevyo. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba makundi yaliyotumika zaidi kama vyanzo vya habari ni vyama vya siasa (37%), vikifuatiwa na wagombea (13%), viongozi wa serikali na idara zake (27%), serikali za mitaa (22%), wananchi wa kawaida (20%), na vyombo vya usalama (11%). Hii inamaanisha kwamba vyombo vya habari viliripoti kwa kiasi kidogo mno kuhusu wagombea na sera zao. Uripoti wa vyombo vya habari kuhusu wagombea na sera zao unawawezesha wananchi kufanya machaguo sahihi siku ya uchaguzi. Jedwali lifuatalo hapa chini linaweka wazi makundi yaliyotumiwa na vituo vya redio kama vyanzo vya habari pamoja na asilimia zake:

## Makundi ya vyanzo vya habari




Hata hivyo, vituo vya redio vilitaja vyanzo tofauti vya habari. Baadhi ya vituo vilifanya vizuri sana katika kuwatumia wagombea na wananchi wa kawaida kama vyanzo vyao vya habari. Vituo vya redio ambavyo viliwatumia zaidi wagombea kuliko vituo vingine ni CG FM (49%), Arusha One FM (29%), Sengerema FM (25%), na Mbeya City FM (24%). Wakati vituo vilivyowatumia zaidi wananchi wa kawaida kuliko vituo vingine ni pamoja na Uvinza Community FM (63%), CG FM (79%), El-Olama FM (42%), Dodoma FM (35%), Sengerema FM (25%), Mashujaa FM (29%), Moshi FM (24%), na Nuru FM (24%). Jedwali lifuatalo hapa chini linaonesha namna gani vituo vya redio viliwatumia wagombea na wananchi wa kawaida kama vyanzo vya habari:

| Wagombea na wananchi kama vyanzo vya habari | | |
|---|---|---|
| Redio | Wagombea | Wananchi |
| Wastani | 13% | 20% |
| Arusha One FM | 29% | 17% |
| Bariadi FM | 14% | 10% |
| Bunda FM | 0% | 6% |
| CG FM | 49% | 79% |
| Chalinze FM | 12% | 19% |
| Dodoma FM | 15% | 35% |
| El-Olama FM | 8% | 42% |
| Flamingo FM | 10% | 8% |
| Manyara FM | 13% | 13% |
| Highlands FM | 4% | 21% |
| Ileje FM | 8% | 14% |
| Jamii FM | 8% | 6% |
| Kasibante FM | 13% | 31% |
| Kicora FM | 3% | 7% |
| Sunrise FM | 6% | 13% |
| Mashujaa FM | 7% | 29% |
| Mbeya City FM | 24% | 14% |
| Moshi FM | 8% | 24% |
| Mpanda FM | 18% | 21% |
| Nuru FM | 10% | 24% |
| Pambazuko FM | 33% | 22% |
| Pamoja FM | 6% | 13% |
| Pangani FM | 0% | 5% |
| Kwizera FM | 0% | 18% |
| Sengerema FM | 25% | 25% |
| Rufiji FM | 15% | 20% |
| Ruvuma FM | 22% | 8% |
| SG FIVE FM | 0% | 23% |
| Standard FM | 13% | 8% |
| TBC Taifa | 8% | 13% |
| TK FM | 7% | 17% |
| Uvinza Community FM | 0% | 63% |
| Uyui FM | 16% | 19% |
| VOS FM | 9% | 11% |
| Vwawa FM | 20% | 8% |


### 4.1.7 Wanawake kama vyanzo vya habari

Ujumuishaji wa wanawake kama vyanzo vya habari ni suala muhimu kwani linatuhakikishia ushirikishwaji wa jinsi husika na hivyo kutubainishia masuala ambayo lazima yatapaswa kuibuliwa kutokana na mlengo wa wanawake. Mwaka 2024, vituo vya redio havikutoa kipaumbele kwa wanawake kama vyanzo vyao vya habari. Utafiti umebaini kwamba 62% ya kazi zilizochunguzwa hazikuwa na mwanamke yeyote aliyetumika kama chanzo cha habari, 23% zilikuwa na mwanamke mmoja kama chanzo cha habari na 15% zilikuwa na wanawake wawili au zaidi kama vyanzo vya habari. Jedwali lifuatalo linaonesha wanawake walivyotumiwa na vituo vya redio kama vyanzo vya habari:




Ikilinganishwa na tafiti zilizotangulia, kipengele muhimu cha kuwajumuisha wanawake kama vyanzo vya habari hakijaimarika. Tukilinganisha takwimu, "kuwa na angalau mwanamke mmoja kama chanzo cha habari" hali ya utendaji wa redio na asilimia zake kwenye mabano ilikuwa kama ifuatavyo: 2018 (43%), 2019 (36%), 2022 (44%), na 2024 (38%).

## Angalau chanzo kimoja cha kike kwa miaka iliyopita





*Chanzo: Yearbook 2018, 2019, 2022 and 2024*

### 4.1.8 Kupiga simu na kutuma ujumbe mfupi wa maneno

Kupiga simu na kutuma ujumbe mfupi wa maneno ni kitu muhimu katika kuonesha ushiriki wa wananchi kwenye mchakato wa uchaguzi. Vyombo vya habari lazima viandae vipindi ambavyo vitawahamasisha wananchi kupiga simu na kutuma ujumbe mfupi wa maneno ili kuwahoji wagombea au viongozi wa vyama vya siasa. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba ushiriki wa wananchi kupiga simu na kutuma ujumbe mfupi wa maneno ulikuwa mdogo 5% kwa kupiga simu na 6% kwa kutuma ujumbe mfupi wa maneno, mtawalia.


### 4.1.9 Uripoti wa nafasi mbalimbali

Kama ilivyokwisha elezwa kwenye kipengele kidogo cha “vyanzo vya habari”, kazi zilizoshughulikiwa kwenye sampuli ya utafiti huu mara nyingi hazikuwataja wagombea; kwa ujumla, ni 12% tu ya kazi zilizoshughulikiwa ndizo zilizowataja. Kati ya kazi 126 zilizohusu wagombea, wenyeviti wa vijiji waliripotiwa zaidi ya wengine (kwa 64.3%), wakifuatiwa na wenyeviti wa vitongoji (kwa 10.3%) na wajumbe wa baraza la kijiji (3.2%). Hata hivyo, vituo vya redio vinahitaji mafunzo zaidi yatakayohusu namna ya kuripoti wagombea. Kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, nafasi kama vile “wajumbe wanawake wa kamati za mitaa” na “wajumbe wanawake wa wa mabaraza ya vijiji” hawakutajwa mahali popote. Jedwali lifuatalo hapa chini linaonesha namna vituo vya redio vilivyoripoti nafasi za wagombea:





### 4.1.10 Matokeo ya utafiti kuhusu tathmini za wagombea

Matokeo ya utafiti yaliyowasilishwa kwenye jedwali hapa chini kwamba kazi 871 sawa na 87.9% ya kazi zote zilizoripoti kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hazikuwajumuisha wagombea. Vituo vingi vya redio viliwajumuisha wagombea kwa kiasi kidogo. Hii ina maanisha kwamba vituo vingi vya redio havikutimiza vizuri wajibu wao wa kuwajumuisha wagombea kutoka kwenye maeneo yao, au wagombea wenyewe hawakuona umuhimu wa kutumia vituo vya redio kwa ajili ya kampeni zao. Hata hivyo, ni vituo vichache tu vya redio ambavyo vilikuwa na asilimia za juu ya kazi zilizokuwa na wagombea angalau mmoja, wawili au zaidi kwenye kazi zao. Vituo hivyo ni pamoja na Arusha One FM (25%), CG FM (39%), na Pambazuko FM (19%). Majedwali yafuatayo hapa chini yanaonesha idadi ya wagombea walioripotiwa kulingana na kituo cha redio:




# Idadi ya wagombea kwa kituo cha redio



Kwa kuongezea, ni kazi 51(5%) tu kutoka kwenye sampuli ndizo ziliwataja wagombea wanawake, kazi 10 (1%) ziliwataja wagombea vijana, na kazi 6 (0.6%) tu miongoni mwa sampuli yetu ziliwataja wagombea wenye ulemavu. Hii inamaanisha kwamba uripoti wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ulikuwa wa chini.


### 4.1.11 Uripoti wa maudhui yaliyohusu sera

Vyombo vya habari vinapaswa kuripoti wagombea na sera za vyama vyao ili kuwaelimisha wasikilizaji. Kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapa chini, matokeo ya utafiti yanaonesha 56.6% ya kazi zilizotaja wagombea pia zilijumuisha maudhui yaliyohusu sera za vyama vyao kwa kiasi kidogo (34%), kwa kiasi kikubwa (15%), na kwa kiasi kikubwa sana (6.9%). Hii inaonesha kwamba zaidi ya nusu ya kazi zilizoshughulikiwa zilifanya vizuri kwenye kipengele hiki.





Hata hivyo pameshuhudiwa tofauti kadhaa kati ya kituo na kituo. Baadhi ya vituo vilifanya kazi nzuri ya kuripoti maudhui yanayohusu sera za vyma vya wagombea. Vituo vya redio vilivyofanya vizuri katika kipengele hiki ni Chalinze FM, Dodoma FM, Flamingo FM, Highlands FM, Ileje FM, Jamii FM, Moshi FM, Mpanda FM, Nuru FM, Pambazuko FM, Rufiji FM, na Sengerema FM. Jedwali lifuatalo linafafanua zaidi:

# Uripoti wa Sera kwa kila kituo cha redio



Kwa ulinganisho, kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 vyombo vya habari vilifanya vizuri katika kipengele hiki, kukiwa na asilimia 60% ya kazi zilizokuwa na maudhui yaliyohusu wagombea na sera za vyama vyao.


**Uripoti wa Sera kwa mwaka 2019**




### 4.1.12 Mafanikio

Kwenye kampeni za uchaguzi, kuyataja mafanikio ya mgombea wakati akiwa madarakani kunawawezesha wapiga kura kufahamu kuhusu uwezo wa wagombea wanaogombea nyadhifa mbalimbali na hivyo kuwawezesha wapiga kura kuwachagua wagombea kwa usahihi. Mwaka 2024, ni 8% tu ya kazi zilizochunguzwa ndizo zilizoripoti mafanikio ya wagombea wakati wakiwa madarakani. Zaidi ya asilimia 90% ya kazi zilizohusu wagombea hazikuripoti kuhusu mafanikio yao.


**Uripoti wa mafanikio ya wagombea**



Hata hivyo, Bunda FM, CG FM, Dodoma FM, Kasibante FM, Mbeya City FM, Mpande FM; Nuru FM, Pambazuko FM, Sengerema FM, na Ruvuma FM waliweza kuripoti mafanikio ya wagombea. Mwaka 2019, hali ya uripoti wa mafanikio ilikuwa bora zaidi (30%) ikilinganishwa na mwaka 2024, japo kwa kazi tatu tu zilizokuwa zimeripotiwa.

### 4.1.13 Kutofanikiwa/kushindwa


Vyombo vya habari kuripoti kuhusu kutofanikiwa kwa mgombea fulani ni jambo muhimu mno kwani linawawezesha wapiga kura kuuelewa udhaifu wa mgombea husika. Mwaka 2024, ni kazi tatu tu (3) ndizo zilizoripoti japo kwa kidogo kuhusu kutofanikiwa kwa wagombea. Hii ina maanisha kwamba, wakati wa uripoti wake, vyombo vya habari havikuwachunguza wagombea kwa kina.




Kazi zilizoripoti kuhusu kushindwa ziliripotiwa na Kasibante FM (mgombea mmoja) na kwenye taarifa ya habari ya Nuru FM (wagombea wawili).

### 4.1.14 Urejeleaji kwenye ilani za uchaguzi za vyama

Vyombo vya habari kuripoti kuhusu wagombea na kuzirejelea ilani za uchaguzi za vyama vyao ni jambo muhimu kwa sababu huwaelimisha wananchi. Kwa mwaka 2024, angalau 30% ya vyombo vya habari vilirejelea ilani za uchaguzi za vyama kwenye uripoti wake. Asilimia kama hiyo (30%) ya vyombo vya habari vilirejelea ilani za uchaguzi za vyama kwenye uripoti wake kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 japo kwa kazi tatu tu wakati kwa mwaka 2024 ilirejelewa kwenye kazi 74 zilizofanyiwa uchunguzi. Jedwali lifuatalo linaonesha asilimia ya urejeleaji kwenye ilani za uchaguzi za vyama.




### 4.1.15 Haiba za wagombea

Ripoti za vyombo vya habari kuhusu haiba za wagombea huwasaidia wapiga kura kuwahukumu wagombea kulingana na sifa zao, ikiwa ni pamoja na uzoefu, uaminifu, uadilifu, huruma na uwezo wa kuongoza. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, kwa mwaka 2024 ni 12% tu ya kazi zilizoshughulikiwa zilitaja haiba za wagombea wakati kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 masuala ya haiba za wagombea yaliripotiwa katika kazi mbili, ambazo ni sawa na asilimia 20%.


### 4.1.16 Matokeo ya utafiti kuhusu uripoti wa vyama vya siasa

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba vyombo vya habari vinawajibika kuzalisha kazi sahihi, zinazozingatia weledi kitaaluma, na bila upendeleo kwa vyama vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi. Kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapa chini, CCM na CHADEMA walipata karibu alama sawa, ikiwa ni 55 (5.5%) na 53 (5.3%) mtawalia. CUF na ACT Wazalendo walifuatia kwa uchache (14% na 13%). Hata hivyo, hili linapaswa kutazamwa kwa kuzingatia taarifa za usuli kwani wagombea wametajwa kwa uchache kwenye kazi husika za kihabari.




### 4.1.17 Mitazamo isiyo au inayowaunga mkono wagombea

Mitazamo humaanisha tofauti za kimaoni kuhusu suala fulani mahsusi, kimsingi ni mielekeo mbalimbali au misimamo ambayo vikundi tofauti vinaweza kuwa nayo kuhusu mada inayoripotiwa. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa uripoti unaozingatia maoni ya watu ni kama haukuonekana kabisa. Hata maoni yanayounga mkono wagombea yalikuwa nadra sana kuonekana, yakiwa kati ya 14% na 11%. Ilikuwa vigumu hata kuona tofauti yoyote kati ya CCM na CHADEMA.



### 4.1.18 Maadili


Wakati wa uchaguzi, haki ya kujibu ni haki ya kujitetea binafsi dhidi ya ukosoaji wa watu kwenye habari hiyo hiyo ambamo ukosoaji ulitangazwa. Kuhusu haki ya kujibu, matokeo yanaonesha kwamba utendaji wa vituo vya redio kwenye eneo hili unakatisha tamaa kwa 37.5%.



## 4.2 NGAZI YA 2: Matokeo kwa vituo vya redio vyenye leseni za wilaya, mkoa na za kijamii


### 4.2.1 Sampuli

Sampuli yetu ilikuwa na vituo 26 vya redio zenye leseni za wilaya, au mkoa, vituo vinane vya redio vyenye leseni za kijamii na kituo kimoja cha utangazaji chenye leseni ya kitaifa, TBC Taifa. Kwa hali ilivyo, kazi nyingi zilizoshughulikiwa kwenye utafiti huu zilitoka kwenye vituo vya redio vyenye leseni za wilaya/mkoa (74%), zilizobaki zilitoka kwenye redio zenye leseni za kijamii (22%), na kutoka kituo kimoja cha utangazaji chenye leseni ya kitaifa (4%).




### 4.2.3 Aina ya kazi za kihabari

Utafiti haujaona utofauti wowote kati ya redio zenye leseni za wilaya/mkoa na zile za kijamii kwenye kuchagua habari na vipindi; vyote vilikuwa na 31% kwa vipindi na asilimia 69% kwa habari.





### 4.2.4 Aina ya kazi

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa hakuna utofauti kati ya habari na makala. Redio za wilaya/mkoa na redio za kijamii zilipata 69% kwenye habari na makala. Kwenye mahojiano, redio za kijamii zilikuwa na mahojiano mengi zaidi kwa 11% ikilinganishwa na redio za wilaya/mkoa zilizokuwa na 8%. Zaidi ya hayo, kwenye majadiliano, redio za wilaya/mikoa zilifanya vizuri (5%) ikilinganishwa na redio za kijamii zilizopata 3%.



### 4.2.5 Muktadha wa uripoti

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba redio za wilaya/mkoa zilitumia zaidi jitihada binafsi (52%) katika kuripoti habari ikilinganishwa na redio za kijamii, ambazo zilikuwa na 42% kwenye kipengele hiki. Hata hivyo, matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa redio za kijamii zilitegemea zaidi habari za matukio na matamko rasmi yaliyoandaliwa ili kuandika habari zao, kwa asilimia 37% na 13.2% mtawalia, kuliko redio za mikoa/wilaya (33.2% na 8.2%, mtawalia). Hata hivyo, vituo vya redio za kijamii na vile vya wilaya/mkoa vilikuwa karibu sawa kwa viwango vya chini vya jitihada binafsi za kutafuta habari kwa 47.5% na 50%, mtawalia. Jedwali la 31 linafafanua zaidi utendaji linganishi katika muktadha wa kuripoti.





### 5.0 Uripoti unaozingatia mada

Kama ilivyokuwa kwenye ngazi ya 1, utafiti huu ulihusu uchaguzi; na kwa hiyo mada kuu ni uchaguzi kwa kila aina ya redio. Hata hivyo, redio za kijamii pia ziliripoti kuhusu mada nyingine kwa 4%, ikilinganishwa na redio za wilaya/mkoa, zilizoripoti masuala mengine kwa 1%. Mada nyingine ambazo ziliripotiwa na redio za kijamii ni masuala ya uharifu na migogoro ya ardhi.


### 5.1 Vyanzo vya habari

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba redio za kijamii zimefanya vibaya kwenye eneo la vyanzo vya habari ikilinganishwa na redio za wilaya/mikoa. Redio za kijamii zimepata 24% na asilimia 21% kwenye kutumia vyanzo vya habari 2-3 na vyanzo vya habari 4+ mtawalia, ilihali redio za wilaya/mikoa zilipata 28% na 26% kwenye kutumia vyanzo vya habari 2-3 na vyanzo vya habari 4+ mtawalia. Lakini utofauti ni mdogo na usiokuwa bainifu. Suala la redio za kijamii kutumia vyanzo vya habari vichache linaweza likahusishwa na kutumia zaidi matukio na matamko rasmi ili kupata habari.




### 5.1.2 Wanawake kama vyanzo vya habari

Matokeo ya utafiti yameonesha tofauti ndogo kuhusu wanawake kutumika kama vyanzo vya habari. Asilimia 61% hadi 62% ya kazi zote zilizochunguzwa hazikuwa na mwanamke kama chanzo cha habari. Hata hivyo, redio za kijamii zilikuwa na baadhi ya kazi ambazo ndani yake kulikuwa na mwanamke mmoja aliyekuwa kama chanzo cha habari lakini kulikuwa na kazi chache ambamo wanawake walitumika kama vyanzo vya habari. Kwa hiyo, utofauti ni mdogo. Tazama jedwali hapa chini:




### 5.1.3 Makundi ya vyanzo vya habari

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba redio za wilaya na mikoa hutumia zaidi vyama vya siasa, viongozi wa kiserikali, viongozi wa serikali za mitaa na tawala zake na wananchi kwa ujumla kama vyanzo vyao vya habari.



## 6.0 Wapiga simu

Matokeo yanaonesha kwamba 95% ya aina zote mbili za redio hazikuwa na wapiga simu kabisa. Hali hii inaonesha kwamba wananchi hawakupewa nafasi ya kuibua hoja na masuala yao kuhusiana na wagombea.

## 7.0 Matokeo ya utafiti kwenye uchunguzi wa wagombea

Utendaji wa chini wa redio za kijamii vile vile unaonekana kwenye idadi ya wagombea. Redio hizo zinawasilisha wagombea kwa (12%) kuliko redio za wilaya/mikoa ambazo zina 13%. Hata hivyo, utofauti ni mdogo na usio onekane bayana.


**Uripoti wa wagombea**

Uripoti wa wagombea kwa makundi ya vituo vya redio

| | Vituo vyenye leseni ya mkoa/wilaya | Redio za Jamii | Jumla/ Wastani |
|---|---|---|---|
| Hakuna chanzo | 87% | 90% | 87.7% |
| Chanzo 1 | 4.9% | 5.5% | 5% |
| Vyanzo 2-3 | 5.3% | 4.1% | 5% |
| Vyanzo 4+ | 2.7% | 0.5% | 2.2% |


## 8.0 Uripoti wa maudhui yanayohusu sera

Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba vituo vya redio za kijamii vilifanya vizuri katika kuripoti maudhui yaliyohusu sera za wagombea kwa asilimia 78% ikilinganishwa na redio za wilaya/mikoa ambazo zilipata asilimia 50%. Matokeo yanaendelea kuonesha kwamba redio za kijamii zimefanya vizuri kuliko redio za wilaya/mikoa katika vipengele vingine vyote vilivyohusu kuripoti sera za wagombea (tazama asilimia kwenye jedwali lifuatalo hapa chini). Haya ni matokeo muhimu sana. Hii inaweza kutafsiriwa kwamba vituo vya redio za kijamii vimetekeleza jukumu la redio katika kuwaelimisha wananchi kuhusu wagombea kwa namna iliyo nzuri kuliko vituo vingine vya redio. Tazama jedwali hapa chini:



## 9.0 Kurejelea ilani za uchaguzi za vyama

Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba vituo vya redio za kijamii vilifanya vizuri katika kiripoti maudhui kwa kurejelea ilani za uchaguzi za vyama kuliko ilivyokuwa kwa vituo vya redio vya wilaya/mkoa. Vituo vya redio za kijamii vilipata 40% ikilinganishwa na vituo vya redio vya wilaya/mkoa vilivyo-pata 32%.




## 10.0 Mafanikio ya wagombea


Matokeo yanaonesha kwamba ilikuwa vigumu kuuona utofauti katika uripoti kati ya aina hizo mbili za redio kuhusu mafanikio ya wagombea. Kila kituo cha redio kilipata karibia 10%. Kwa ujumla, uripoti wa mafanikio ya wagombea ulikuwa mbovu kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:

**Uripoti wa mafanikio ya wagombea**

| | Vituo vyenye leseni ya mkoa/wilaya | Redio za jamii | Jumla |
|---|---|---|---|
| Hakuna uripoti wa mafanikio | 91% | 90.5% | 219 |
| Ndio, kidogo | 3.5% | 2.4% | 8 |
| Ndio, sana | 3.0% | 7.1% | 9 |
| Ndio, kwa kiasi kikubwa | 2.5% | 0.0% | 5 |


## 10.1 Kushindwa kwa wagombea

Matokeo yanaonesha kwamba redio za kijamii hazikuwahi kabisa kujadili kuhusu kushindwa kwa wagombea ikilinganishwa na redio za wilaya/mkoa ambazo zilipata asilimia 2%. Kushindwa kwa wagombea kumetajwa mara tatu kwenye kazi mbili tu: moja kutoka Kasibante FM na nyingine kutoka Nuru FM. Kwa ujumla, matokeo yaliyomo kwenye jedwali hapa chini yanaonesha kwamba aina zote mbili za redio zilifanya vibaya kwenye kipengele hiki.




## 10.2 Haiba za wagombea

Haiba za wagombea ni muhimu mno kwani wakati fulani wapiga kura hufanya maamuzi kulingana na tabia binafsi za mgombea bila kujali sera. Matokeo yanaonesha kwamba redio za kijamii ziliripoti vizuri zaidi kuhusu haiba za wagombea kwa 17% ikilinganishwa na redio za wilaya/mkoa zilizokuwa na asilimia 12%. Hata hivyo, tofauti hizi siyo kubwa sana.





## 10.3 Matokeo kuhusu uripoti wa vyama vya siasa vya wagombea

Matokeo yanaonesha utofauti mkubwa na bayana kati ya redio za wilaya/mkoa na redio za kijamii kuhusu uripoti wa vyama vya siasa vya wagombea. Redio za kijamii ziliweka kipaumbele katika kuripoti upande wa upinzani, hasa CHADEMA (kwa 65%) na CUF (56%). Redio hizo ziliripoti kidogo kuhusu CCM (22%). Hata hivyo, redio za wilaya/mkoa ziliripoti kwa uwiano sawa kwenye kipengele hiki. Kwa kuongezea, hapakuwa na usawa katika kuvitaja vyama vya upinzani (CUF na ACT Wazalendo). Wakati aina zote mbili za redio ziliwataja kwa usawa wagombea wa CUF, wagombea wa ACT Wazalendo walitajwa mara moja tu na redio za wilaya/mkoa na mara moja tu wakitajwa na redio za kijamii. Huenda ikawa ACT Wazalendo haikuwa na wagombea mahsusi kwenye maeneo husika, lakini takwimu zinaonesha utofauti mkubwa na wa wazi kwa vyama vyote vya siasa.

## 10.4 Mitazamo


Matokeo yanabainisha kwamba vituo vya redio za kijamii vilielezea kwa uchache kuhusu mitazamo zikipendelea zaidi wagombea wa CCM kwa (8%) ikilinganishwa na redio za wilaya/mkoa ambazo zilipendelea zaidi wagombea wa CCM kwa asilimia 16%. Hata hivyo, hapakuwa na utofauti wowote mkubwa uliooneкana kati ya redio za wilaya/mkoa na vituo vya redio za kijamii viliporipoti kuhusu wagombea wa CHADEMA kwenye kipengele hiki. Viliripoti kuhusu wagombea wa CHADEMA kwa 12% na asilimia 9% mtawalia.







## 10.5 Kuuliza Maswali magumu

Kuuliza maswali magumu kunamuwezesha muendesha mahojiano kupata picha kamili au kupata maana kamili ya kinachosemwa. Kuhusiana na kuuliza maswali, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba redio za wilaya/mkoa zilifanya vizuri katika kuwahoji wagombea wa CCM kwa 70% ikilinganishwa na asilimia 0% ambayo redio za kijamii zilipata katika kipengele hiki.





Kuhusu wagombea wa CHADEMA, redio za kijamii ziliwahoji wagombea wa chama hicho kwa kiasi kikubwa kwa asilimia 60% kuliko wagombea wa CCM ambao waliohojiwa kwa 40%. Hata hivyo, utofauti huo haukuwa mkubwa sana.




## 10.6 Maadili

Hakuna utofauti wowote kati ya aina hizo mbili za redio kuhusiana na haki ya kujibu. Pande zote mbili hazikufanya vizuri kwenye eneo hili (2/3) katika habari zao muhimu.



# 11.0 NGAZI YA 3: Matokeo ya kituo cha utangazaji cha Taifa—TBC Taifa

## 11.1 Sampuli

***TBC Taifa*** ilichangia kazi 39 kwenye sampuli. Kwa sehemu kubwa redio ya taifa inatangaza habari (81%) na vipindi vichache. TBC Taifa ilitumia habari na makala tu na si majadiliano au mahojiano.

## 11.2 Vyanzo vya habari

Kuhusiana na idadi ya vyanzo vya habari, kituo cha utangazaji cha Taifa kilifanya karibu sawa na wastani uliobainishwa kwenye 4.3 huko juu. Kwenye kuwatumia wagombea na wananchi wa kawaida kama vyanzo vya habari, TBC Taifa imefanya vibaya ikiwa ni chini ya wastani kwa 8% na asilimia 13%, mtawalia.

## 11.3 Uripoti wa wagombea

Matokeo yanaonesha kwamba TBC Taifa haikumtaja mgombea yeyote kwenye asilimia 92% ya kazi zake zilizochambuliwa kwenye utafiti huu. Hali hii kwa TBC Taifa inaeleweka, kwa kuzingatia kwamba TBC Taifa, ni kituo cha utangazaji cha taifa, hakina sababu ya kumtaja mgombea mmoja kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. TBC Taifa iliwasilisha kazi tatu tu ambazo zilikuwa na habari kuhusu wagombea, mara mbili ikiwa na wagombea wawili na mara moja ikiwa na wagombea watatu na hivyo kufanya jumla ya wagombea saba.

## 11.4 Tathmini ya wagombea

Hivyo, kwenye uchunguzi ufuatao, tunapaswa kukumbuka kwamba wakati tunafanya uchambuzi wetu kuhusu TBC Taifa tunarejelea kwenye kazi tatu zenye wagombea saba. Kuhusiana na uripoti unaohusu sera, TBC Taifa iliripoti kidogo kwenye eneo hili kwa wagombea sita kati ya saba na hapakuripotiwa chochote kwa mgombea mmoja. Kituo hakikumtaja mgombea yeyote wala ilani za uchaguzi za vyama vyao. Pia haikuripoti chochote kuhusu mafanikio, kushindwa na haiba za wagombea. Kituo kilijitenga na kuchambua vipengele hivyo.

Hali ilikuwa hivyo hivyo kwa mitazamo inayounga au isiyiounga mkono mgombea yeyote. Kwenye uripoti wa TBC Taifa hapakuwa na mitazamo yoyote. Zaidi ya hapo, TBC Taifa haikuwa na mahojiano wala majadiliano na wagombea na hili linaeleweka pia ikizingatiwa kwamba hiki ni kituo cha kitaifa na kwa hiyo kisingeweza kumudu kuwafikia wagombea wote (Tazama idadi ya wagombea hapo juu).

# 12.0 UFUATILIAJI WA WAKATI HALISI

## 12.1 Kwa ufupi

Kwenye YB ya mwaka 2024, tulianzisha mbinu mpya inayoitwa 'Ufuatiliaji wa Wakati Halisi'. Ni wazo jipya ambalo halikutumika kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 na kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020; ilifanyiwa majaribio kuanzia tarehe 11 Novemba mpaka tarehe 01 Disemba, 2024. Ufuatiliaji ulisimamiwa na Wafuatiliaji wa mikoa ambao walipewa kazi ya kufuatilia vituo mahsusi vya redio kwenye mikoa teule na kusimamiwa na Wafuatiliaji wa kanda waliokuwa na wajibu mkuu wa kudhibiti ubora kwenye kanda zao. Wafuatiliaji wa kanda waliripoti kwa wafuatiliaji wa kitaifa. Wafuatiliaji wa mikoa waliwasilisha ripoti za kila siku kwa wafuatiliaji wa kitaifa kupitia teknolojia ya KoboToolbox baada ya Wafuatiliaji wa kanda kujiridhisha na kazi iliyofanyika. Ufuatiliaji huu ulijihusisha na masuala manne tu: uripoti wa wagombea (kwa lengo mahsusi la kuangalia wagombea wanawake, vyanzo vya habari (wananchi, vijana, wanawake na Mamlaka za Serikali za Mitaa), uripoti kuhusu vyama vya siasa na masuala ya kimaadili. Wafuatiliaji walikuwa wakifanya vikao vya mtandaoni mara moja kwa wiki ili kujadili zoezi la ufuatiliaji na changamoto zilizokuwa zikijitokeza wakati wa utekelezaji wa zoezi hilo.

## 12.3 Mafunzo na utekelezaji wa majukumu

Kabla ya zoezi la ufuatiliaji halijaanza, wafuatiliaji walifundishwa kwa vitendo jinsi ya kutumia muongozo wa ufuatiliaji, walipewa ratiba ya vipindi vya redio na kuunganishwa na ama Meneja wa

kituo au meneja wa vipindi. Wafuatiliaji walipaswa kufuatilia taarifa ya habari ya jioni na vipindi vitatu kwenye kituo cha redio alichopangiwa kulingana na uwepo wa kipindi husika kwenye ratiba ya vipindi na waliongozwa na miongozo ya ufuatiliaji. Walitoa mrejesho wa kila siku, kwa njia ya simu, kwenye vituo vya redio ambavyo vilihitaji maboresho na kwenye maeneo ambayo uripoti ulikuwa mzuri, kuwatia moyo ili kuendelea kusimamia viwango. Kwa ujumla, vituo 20 vya redio vilifuatiliwa ambavyo ni Arusha One FM, Bariadi FM, CG FM, Dodoma FM, Manyara FM, Highlands FM, Kahama FM, Kasibante FM, Mbeya City FM, Mpanda FM, Pambazuko FM, Abood FM, Kwizera FM, Sengerema FM, Ruvuma FM, Sunrise FM, Pangani FM, TBC Taifa, TK FM, na Vos FM.

## 12.4 Tulichokibaini

Kama ilivyokuwa, majaribio hupima ni kwa namna gani kazi husika ingefanyika na kupokelewa na vituo vya redio, katika majaribio haya tuliweza kubaini yafuatayo:

- Jitihada hizi zilipokelewa kwa mtazamo chanya na vituo vya redio, ingawa kwa baadhi ya vituo, suala la kutoa mrejesho wa kila siku kuhusu maeneo yaliyohitaji maboresho waliona kama ni kufanya upolisi kwa uandishi wao wa habari. Hata hivyo, hali hii ilikuwa na mafanikio chanya. Wafuatiliaji walibaini kwamba, kwa siku fulani fulani, baadhi ya vituo vya redio vilibadilisha mpangilio wa vipindi vyao ili kuendana na malengo ya mradi wakati fulani vituo vya redio viliwapigia simu wafuatiliaji ili kuwajulisha kwamba wasingeweza kutangaza kipindi fulani kwenye siku mahsusi kwa sababu wasingeweza kupata vyanzo vyao mbalimbali vya habari

- Mrejesho uliotolewa na vituo vya redio ulitofautiana baina ya kituo kimoja na kingine: vichache viliweza kuendana na kutekeleza mabadiliko, lakini vingi vilifanya taratibu sana kupokea mabadiliko (ilichukua siku kadhaa), na vingine vichache vilihitaji muda zaidi kuyafanyia kazi maoni (ilichukua muda mrefu).

- Matokeo ya ufuatiliaji yalijibainisha waziwazi kwenye eneo la vyanzo vya habari kwenye vipindi, hasa kwa kuvikumbusha mara kwa mara vituo vya redio kuhakikisha vinakuwa na wagombea wawili kwenye vipindi vyao bila kusahau ujumuishaji wa sauti za wananchi na wanawake. Hili linaonekana kwenye eneo la matokeo (Tazama hapo juu), ambapo vituo vya redio kama vile CG FM, Highlands FM, Pambazuko FM, Kasibante FM, Mpanda FM, na Sengerema FM vimefanya vizuri zaidi kwenye kutumia vyanzo vingi vya habari.

- Vituo vya redio kuwapa kipaumbele zaidi viongozi wa kitaifa na mikoa kwa gharama ya wanasiasa wa eneo husika kwa namna fulani jambo hili linaonesha sababu ya wagombea kupata uripoti wa chini sana (12% tu). Vyama vikubwa vya siasa vilitumia viongozi wao wa kitaifa na mikoa kufanya kampeni kwa ajili ya wagombea wao kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, na vituo vingi vya redio vilipendelea kutumia majina maarufu huku wakiwasahau watu halisi watakaopiga kura. Kusingekuwa na zoezi la ufuatiliaji, tunaamini kwamba asilimia za uripoti katika eneo hili ungekuwa wa chini zaidi.

- Wakati wa ufuatiliaji wetu, ilikuwa vigumu kuuona uripoti wa vijana na watu wenye ulemavu. Ilibainika kwamba vituo vingi vya redio havina utamaduni wa kuvitambulisha vyanzo vyao vya habari ama kwa umri, hali ya ulemavu au kama wanatoka kwenye jamii au mashirika ya watu wenye ulemavu. Hali hii ya kukosekana kwa utambulisho mzuri, iliufanya utambulisho wa vyanzo vya habari kuwa mgumu zaidi hasa hasa kwa vijana na watu wenye ulemavu labda itokee kwamba kipindi husika kiwe kinahusiana moja kwa moja na makundi haya. Wafuatiliaji wetu waliendelea kuvikumbusha vituo vya redio kuhakikisha vinatafuta namna ya kuyatambulisha makundi haya ili kuufanya utambulisho kuwa rahisi.

- Vituo vingi vya redio vililalamika kuwa vina idadi ndogo ya wafanyakazi, jambo ambalo lilikwamisha kufikiwa kwa matamanio yao ya kuboresha uripoti wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Hali hii imekuwa changamoto sugu inayovikabili vituo vingi vya redio nchini, huku kukiwa na baadhi ya vituo vya redio vikiwa na wafanyakazi mpaka watano kwa kituo kizima. Bado walitakiwa kufanya kazi kwa saa 24 kwa siku na kuzalisha vipindi bora vinavyochochea mijadala ya kijamii na hatimaye kuwa na jamii yenye ufahamu.

- Kwa kutekeleza majaribio ya ufuatiliaji wa wakati halisi kwenye mradi wa YB 2024 kuhusu uchaguzi umetupa ufahamu mzuri

Kwenye vipindi, vijana wanawasilishwa kama wapiga kura, na si kama watu wanaoweza kugombea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Ufuatiliaji wetu unaonesha kwamba kwenye vipindi vingi vinavyowahusu vijana, vijana wanaonekana kama wapiga kura na si vijana kama viongozi. Mtazamo huu, unajenga mtazamo potofu ambao hauwanufaishi vijana ambao ndio wengi. Vituo vya redio vinapaswa kupambana kuweka ulingalifu kwenye uripoti wao na kisha kuwaweka vijana waonekane kama wapiga kura na vilevile kama viongozi.

- Vituo vingi vya redio vilikuwa hai zaidi siku ya uchaguzi, vikituma waandishi kwenye vituo vya kupigia kura, vikiwahoji wananchi na kuripoti matokeo ya uchaguzi. Kulikuwa na uripoti mzuri zaidi siku hii ikilinganishwa na siku zilizotangulia.

sana kuhusu hali ya uandishi wa habari wa redio kwenye mikoa yote iliyofanyiwa utafiti. Wakati kwa ujumla wake, vituo vya redio viliupokea kwa mtazamo chanya utaratibu huu, utaratibu huu pia uliweza kubainisha changamoto kadhaa muhimu zinazohitaji kufanyiwa kazi, zikiwamo mapokeo ya taratibu ya mrejesho kutoka kwa wafuatiliaji na mambo ya kupendelea zaidi viongozi wa kitaifa kuliko wale wa maeneo husika jambo ambalo lilizuia uripoti mzuri wa wagombea wa maeneo husika wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Matokeo yanaonesha uhitaji wa haraka kwa vituo vya redio kuboresha upatikanaji na utumiaji wa vyanzo vyao vya habari ili kuboresha utamaduni unaotoa kipaumbele kwa ujumuishi wa vyanzo vya habari, hasa hasa kutoa nafasi kwa vijana na watu wenye ulemavu. Zaidi ya hapo, suala la upungufu wa wafanyakazi kwenye vituo vingi vya redio linamaanisha panahitajika msaada mkubwa na rasilimali za kutosha ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao vizuri nyakati za uchaguzi. Kwa ujumla, zoezi hili la ufuatiliaji linathibitisha hatua muhimu iliyofikiwa kuelekea kwenye maboresho ya ubora katika uripoti wa habari zinazohusiana na uchaguzi kwenye vyombo vya habari, na kuongeza raia wenye ufahamu, kuweka msingi wa mipango ya baadaye ili kuimarisha demokrasia na uwakilishi.

## 13.0 MITAZAMO YA WADAU KUHUSU MATOKEO YA UTAFITI HUU

Mbali na uchambuzi wa kuzingatia namba na takwimu, mradi wa Yearbook hutoa nafasi kwa ufahamu wa maelezo kuongeza thamani kwenye uchambuzi wa namba na takwimu. Ufahamu huu ulipatikana kwa kuwashirikisha wadau, ambao ni mameneja wa vituo vya redio, mameneja wa vipindi, na wawakilishi kutoka mashirika yanayojihusisha na habari, ambao mitazamo yao iliweza kuongeza mwanga kwenye tafsiri iliyopatikana kwenye uchambuzi wa namba na takwimu. Kwa hiyo, sehemu hii, inajibu swali muhimu lifuatalo: "Kwa mujibu wa mtazamo wa wadau, ni kipi kinafafanua ubora wa uripoti wa vituo vya redio kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024? Kwa ujumla, tuliwahoji wadau 17 nchini kote.

### 13.1 Uripoti wa wagombea

Katika kujibu suala la ukosefu wa uripoti wa kina kuhusu wagombea uliofanywa na vituo vya redio, Meneja wa vipindi wa Sengerema FM alifafanua kwamba, kwa sehemu kubwa wagombea walikuwa hawapatikani na kwamba maafisa uchaguzi hawakuwapa waandishi wa habari majina ya wagombea. Kwa mfano, kule Sengerema, ni wagombea wa CCM na CHADEMA tu ndio waliokuwa wanafahamika. Kinyume chake, wagombea kutoka vyama vingine, kama vile NLD, NCCR Mageuzi, na ACT Wazalendo, walikuwa hawafahamiki na jamii. Wagombea hawa hata kampeni zao hawakufanya, hali iliyowaacha wapiga kura wakutane na majina yao kwenye karatasi ya kupigia kura.

Kutoka Ukerewe, Meneja wa Flamingo FM alieleza kwamba wagombea walikuwa na ufahamu mdogo kuhusu namna ya kutumia vyombo vya habari kikamilifu kwa ajili ya kampeni zao za kisiasa. Walipendelea zaidi kampeni za nyumba kwa nyumba kuliko kutumia vyombo vya habari. Meneja wa Flamingo FM alitanabaisha kwamba hata viongozi wa wilaya walionekana kupendelea zaidi kutumia televisheni ya taifa, mara nyingi wakikodi waandishi kutoka Mwanza na kisha kuwalipa ili kuripoti habari zao badala ya kufanya kazi na vituo vya redio vya eneo husika.

Sababu tatu zilihusishwa na uripoti mdogo wa wagombea: kutokuaminiana kati ya wagombea na vyombo vya habari, ufupi wa muda wa kampeni, na changamoto za kifedha zinazovikabili vituo. Akitoa maoni kuhusu kutokuaminiana, mshiriki mmoja alitanabaisha kwamba baadhi ya wagombea walikuwa na mtazamo hasi dhidi ya vituo vya redio vinavyomilikiwa na halmashauri za wilaya. Walidai kwamba uendeshaji wa vituo hivi vya redio ulikuwa na upendeleo uliokinufaisha zaidi chama tawala (CCM). Matokeo yake, baadhi ya wagombea wa

vyama vya upinzani walikuwa hawataki kuhojiwa au kuvitumia vituo hivyo vya redio.

Zaidi ya hapo, mshiriki aliongezea kwamba muda wa kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ulikuwa mchache, ukianzia Novemba 20 mpaka Novemba 26, 2024. Kwa mujibu wa mshiriki huyu, kipindi cha siku saba kilikuwa kifupi sana kwa vituo vya redio kuweza kuwashirikisha na kutoa fursa sawa kwa wagombea wote waliogombea nyadhifa mbalimbali. Akiongezea mchango wake kwenye suala hili, Mratibu wa TADIO Bwana Cosmas Lupoja, alisisitiza kwamba wiki mbili hazikuwa zinatosha kuviwezesha vyombo vya habari kupanga na kuripoti vya kutosha kuhusu wagombea wote. Kutokana na hali hiyo, vyombo vya habari vilijikita zaidi kwenye nafasi mbili tu, yaani mwenyekiti wa kijiji na mwenyekiti wa serikali ya mtaa.

Changamoto ya kifedha ambayo vituo vya redio vinaipitia pia imetajwa kuwa sababu muhimu iliyokwamisha uwezo wa vituo vya redio kufikisha mawimbi yake kwa wagombea. Washiriki wengi kutoka kwenye vituo vya redio na TADIO walibainisha kwamba vituo vya redio nchini vinapitia changamoto kubwa ya kifedha kiasi cha kushindwa hata kuwawezesha kifedha waandishi wao wa habari ili kuhudhuria kampeni za uchaguzi maeneo ya mbali na kituo cha redio kilipo.

Katibu wa chama cha watangazaji wanaojitegemea (National Independent Broadcasters Association-NIBA), Bwana Heavenlight Kavishe, alichangia kwenye hoja hii na pamoja na kutambua uwepo wa changamoto hii, alitoa wito kwa misaada ya kifedha kwa vituo vya ndani vya redio. Aliweka wazi kwamba, isingekuwa rahisi kwa vituo hivi vya redio kuripoti kikamilifu kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa bila msaada ya kifedha. Aliongezea kwamba serikali inapaswa kuelekeza misaada ya kifedha huko ili kuvijengea uwezo vyombo hivi vya habari ili viweze kutekeleza majukumu yao kama kuhabarisha umma na kujenga wananchi wenye ufahamu.

### 13.1.1 Uripoti wa sauti za wanawake na wagombea wanawake

Kuhusu uchache wa sauti za wanawake (siyo wagombea wanawake), baadhi ya washiriki walielezea wasiwasi miongoni mwa wanawake ambao huogopa kutumia vyombo vya habari au kushiriki kwenye mahojiano ya kwenye vyombo vya habari. Wahojiwa walibaini kuwa kuna uwezekano mkubwa kwa wanawake kuepuka kujihusisha na vituo vya redio kuliko wenzao wa kiume. Kwa mujibu wa washiriki hawa, hali hii inahusishwa na mwelekeo wa kiutamaduni na kukosa kujiamini miongoni mwa wanawake wa kawaida maeneo ya mikoani.

Ushiriki wa wagombea wanawake haukuwa tofauti na mahali pengine kwenye utafiti huu. Kama ilivyooneshwa kwenye matokeo ya utafiti hapo juu, uripoti wa wagombea wanawake ulikuwa wa chini, kwa 5%. Japokuwa suala hili linaweza kuhusishwa na uchache wa wanawake waliokuwa wameteuliwa kugombea nyadhifa fulani ikilinganishwa na wagombea wanaume, washiriki kutoka kwenye vituo vya redio walibainisha kwamba wagombea wanawake hawakuwa wakionesha ushirikiano pindi walipoombwa kushiriki mahojiano au majadiliano kwenye vipindi vya redio, na walilihusisha hili na ukosefu wa mbinu za kimkakati za kutumia vyombo vya habari ili kujitangaza kipindi cha uchaguzi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (Tanzania Media Women Association - TAMWA), Dkt. Rose Reuben, alikiri kwamba japokuwa uripoti wa vyombo vya habari kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 kwa ujumla wake ulikuwa umeimarika, bado kulikuwa na wasiwasi kuhusu uwakilishi usiojitosheleza wa kijinsia. Alibainisha kwamba uripoti kuhusu wagombea wanawake na ushirikishaji wa wanawake kama vyanzo vya habari uliendelea kukosekana, alihoji kama waandishi wa habari wanaelewa umuhimu wa kuzijumuisha sauti za wanawake kwenye uripoti wao.

### 13.1.2 Uripoti wa wananchi wa kawaida

Zaidi ya hapo, wananchi wengi wa kawaida wanaogopa kujihusisha na vyombo vya habari. Alitoa uzoefu wake kwamba wananchi wa kawaida wakiombwa kutoa maoni yao huwa wanakataa. Hali hii inaanzia kwenye kuwa na kiwango kidogo cha elimu na kukosa ufahamu wa umuhimu wa kushiriki majadiliano kwa mada zinazohusiana na uchaguzi kwani wengi miongoni mwao wanaamini kwamba ni wasomi tu ndio wenye nafasi ya kutoa maoni yao. Palitolewa wito kuongezwa dozi ya elimu ya uraia ili kuwajengea uwezo wananchi wa kawaida kushiriki mijadala inayohusu uchaguzi.

Vyombo vya habari vilijizuia kuruhusu wananchi wa kawaida kupiga simu kutokana na wasiwasi wa uwezekano wa kuibuka kwa kauli zenye hisia ambazo zingeweza kusababisha shutuma zisizo na msingi dhidi ya wagombea. Kulikuwa na wasiwasi

kwamba kuruhusu wananchi wa kawaida kutoa madai yasiyo na msingi kunaweza kuviweka vituo vya redio hatarini. Ilibainika kuwa baadhi ya watu walipeleka malalamiko binafsi dhidi ya wagombea maalumu, jambo ambalo lingeweza kusababisha wananchi hao kutumia lugha ya dharau wakiwa hewani kama wangepewa nafasi.

Meneja wa vipindi kutoka Chalinze FM alisema, "Uchaguzi ni suala nyeti na vyombo vya habari vinauhisi unyeti huo. Kama tungewaruhusu wananchi wa kawaida kupiga simu na kuwatuhumu au kuwachafua wagombea kituo chetu kingefungiwa mara moja. Kwa hiyo tulichagua kukiondoa kipengele hiki kwenye vipindi vilivyohusiana na uchaguzi." Alipoulizwa kwa nini redio hazikuruhusu kupiga simu kwenye vipindi vilivyohusiana na uchaguzi, Mratibu wa TADIO alifafanua kwamba kutokana na unyeti wa uchaguzi, vituo vya redio viliamua kuachana na kipengele hicho ili kujilinda dhidi ya adhabu ambazo zingeweza kutolewa kutokana na wapiga simu kutojiheshimu wanapokuwa hewani au endapo itatokea vituo vya redio vikashindwa kuweka usawa wa wapiga simu kwa msingi wa vyama vya siasa.

Kwa ujumla, washiriki walisisitiza kwamba vyombo vya habari vinapaswa kuwa vinafikika kwa urahisi na wananchi wa kawaida, ili kuwajengea uwezo wa kujiamini wakati wakizungumza na vyombo vya habari. Licha ya kuwa baadhi ya wananchi wana ufahamu mzuri wa masuala mbalimbali yakiwamo masuala ya uchaguzi, mara nyingi walijikuta wametenganishwa na vyombo vya habari, hali iliyoonekana kuwepo kwa kiwango tofauti.

### 13.1.3 Kuhoji ahadi za wagombea, mafanikio yao na kushindwa kwao

Vituo vya redio kupata tabu kuripoti kuhusu kufanikiwa au kushindwa kwa wagombea kulitokana na kushindwa kujipanga kikamilifu katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kuripoti kuhusu kufanikiwa au kushindwa kufanikiwa kwa mgombea aliyeko madarakani kunawataka waandishi wa habari kutenga muda wa kutosha kukusanya taarifa muhimu kuhusu ahadi ambazo mgombea aliyeko madarakani alizitoa huko nyuma na kuzihoji kama amefanikiwa au ameshindwa kuzitekeleza. Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Bwana Deodatus Balile, alionesha wasiwasi wake, akisema kwamba vyombo vya habari havikuwa vimejiandaa kuripoti kwenye maeneo haya muhimu. "Tukiwa kama wanafamilia ya vyombo vya habari, hatukujadili na kufikia uelewa wa pamoja kuhusu namna ya kuripoti uchaguzi [Uchaguzi wa Serikali za Mitaa], mada gani za kuziangazia zaidi, na ni malengo gani tuliyotaka kuyafikia."

Meneja kutoka Sengerema FM alibainisha kwamba waandishi wengi walioripoti uchaguzi waliweka kipaumbele kwenye habari zilizowapa manufaa wao binafsi. Tulibaini kwamba mara nyingi waandishi wanapendelea kushiriki kampeni za wagombea ambao hutoa marupurupu ya fedha kuliko kujadili kufanikiwa au kushindwa kwa wagombea. Zaidi ya hayo, alieleza kwamba baadhi ya wagombea waliokuwa madarakani walikataa kushiriki mahojiano ambayo yangeweza kuuanika udhaifu wao. Matokeo yake, wandishi waliamua kuachana na habari za namna hiyo ili kudumisha mahusiano ya amani yaliyokuwepo baina yao na wagombea. Ukosefu wa vyombo vya habari kuripoti kuhusu utendaji wa wagombea pia ulihusishwa na kikwazo cha muda, jambo lililofanya iwe vigumu kuripoti vipengele vyote kikamilifu.

Moja ya mafunuo yanayosumbua kuyaelewa na yanayohusiana na kushindwa kwa vituo vya redio kuhoji mafanikio na kushindwa kwa wagombea ni ile hali ya wagombea kukataa kuzungumza na waandishi wa habari. Baadhi ya mameneja wa vipindi walidokeza kwamba waandishi wao kushindwa kulifikia vizuri eneo hili moja kwa moja haikuwa kwa sababu hawakuwa wamejiandaa kuripoti kuhusu uchaguzi au kwamba walikuwa wakitafuta pesa la hasha. Baadhi ya wagombea waliokuwa madarakani kwenye nafasi za wenyeviti wa vijiji na wenyeviti wa mitaa walikuwa wawazi wakisema kwamba hata kama wangependa kushirikiana na vyombo vya habari kujadili mafanikio au kushindwa kwao, walizuiliwa na vyama vyao. Hivyo, wasingeweza kufanya chochote. Kwa kuongezea, baadhi ya vituo vya redio vinavyomilikiwa na wanasiasa kutoka chama tawala-walizuia uripoti unaochimba mambo kwa kina na kuvitahadharisha vituo vyao vya redio kuepuka kuripoti kuhusu wagombea wa vyama vya upinzani.

# 14.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Ripoti hii ilichunguza kwa kina uripoti uliofanywa na vituo vya redio kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 kwa kutumia vigezo vya ubora kwenye aina mbili tofauti za uandishi wahabari. Aina ya kwanza iliangazia kigezo cha ubora wa uripoti kwa ujumla, ikijumuisha muktadha wa uripoti, vyanzo vya habari na uripoti wa kiuandishi wa habari kwa ujumla wake. Huko nyuma, vigezo hivi vilishawahi kutumika kutathmini hali ya uripoti wa vyombo vya habari nchini kwenye

miaka ya 2018, 2019, na 2022. Kategoria ya pili ililenga moja kwa moja kwenye uripoti wa kiuandishi wa habari ulioandaliwa kwa ajili ya kuripoti masuala ya uchaguzi ikijumuisha vigezo kama vile uripoti wa wagombea, maudhui yanayohusu sera, mafanikio na kushindwa kwa wagombea, n.k.

Matokeo ya utafiti huu yanabainisha kwamba uripoti wa vyombo vya habari kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 umeshuhudia maboresho kidogo ikilinganishwa na miaka iliyopita. Kwa ujumla, kuna tabia ya kudumaa kwa kiwango cha chini na, wakati mwingine, kiwango kisichoridhisha cha ubora wa uripoti. Wakati kukiwa na maboresho kiasi kwenye eneo la kutumia vyanzo vingi vya habari, athari ya jumla imebaki kuwa ni ndogo. Aidha, vituo vya redio vimeonesha ongezeko la wastani katika kuchukua hatua ya kuripoti kuhusu masuala muhimu ya uchaguzi; hata hivyo, hii halijatafsiriwa kwa kiasi kikubwa katika uboreshaji mkubwa katika ubora wa uripoti.

Moja ya eneo la wasiwasi ni kuendelea kwa uwakilishi mdogo wa sauti za wanawake kwenye uripoti wa vyombo vya habari. Utafutaji wa mitazamo na ufahamu kutoka kwa wanawake bado hautoshi. Mwelekeo huu unaonesha masuala ya kimfumo ndani ya mazingira ya vyombo vya habari yanavyoendeleza tofauti za kijinsia katika kuripoti.
Kwenye kuchunguza uripoti wa wagombea, iko wazi kuwa pameendelea kuwepo udhaifu mkubwa katika eneo hilo. Uripoti ulikuwa wa chini kiasi cha kushangaza - ni 12% tu ya kazi zote zilizochunguzwa ndio zilijumuisha wagombea. Zaidi ya hapo, ubora wa kazi hizi ulikuwa unakosekana kwenye taarifa muhimu vikiwamo vipengele muhimu kama vile mafanikio ya wagombea katika kipindi cha uongozi wao na kushindwa kwao ambavyo vilikuwa vinakosekana kwenye uripoti uliochunguzwa. Upungufu huu unadhoofisha uwezo wa wapiga kura kuwatathmini wagombea kulingana na rekodi zao na maoni sahihi kuhusu uwezo wa wagombea.

Kwa kuongezea, uripoti uliohusu maudhui ya sera za wagombea bado umeonekana kutojitosheleza. Bila uchunguzi thabiti wa sera za wagombea, wapiga kura wanaachwa bila nguvu na wanakosa taarifa muhimu. Kukosekana kwa mitazamo mbalimbali, hasa kutoka kwa wananchi na wataalamu wabobezi kunakwamisha uwezo wa wananchi kufanya maamuzi sahihi. Upungufu huu unaonesha pengo lililopo kwenye dhima ya vituo vya redio katika kuwezesha mazingira ya kidemokrasia na wananchi wenye ufahamu.
Kutokana na ufahamu uliopatikana kutoka kwa wadau wa vyombo vya habari, tunahitimisha kwamba, kwa sehemu fulani, matokeo hayo yametokana na sababu za ndani ya vyombo vya habari kama vile ukosefu wa uwezo au nia kwa upande wa waandishi wa habari wa ndani, ukosefu wa msaada kutoka kwa wahariri, au uelewa mdogo wa jukumu la vyombo vya habari katika uchaguzi. Hata hivyo, matokeo hayo pia yamesababishwa na sababu za nje. Mazingira yaliyopo ya kisiasa bado hayawezeshi uwazi ndani ya vyombo vya habari kuhusu uwezo wa wagombea kushughulikia changamoto za wananchi. Ukosefu wa fedha ni kikwazo kikubwa kwa vituo vya redio katika kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Ushawishi unaotumiwa na wamiliki wa vituo vya redio unaweza kuwazuia waandishi wa habari kuwahoji wagombea wa upinzani na kuwasilisha maoni yao. Nguvu hii, iliyounganishwa na utamaduni wa kujidhibiti, inaendelea kuzuia uadilifu wa uandishi wa habari ndani ya mazingira ya vyombo vya habari nchini. Kupuuzwa kwa sauti za wanawake katika taarifa na vipindi vya redio mara nyingi kunatokana na kawaida za kijamii na kitamaduni ambazo zinawakatisha tamaa au kuwanyamazisha wanawake-hasa katika mazingira ya vijijini-kushiriki katika mambo ya umma.
Tukitafakari kuhusu matokeo ya mradi wa Yearbook kwa mwaka 2024, na tunapokaribia Uchaguzi Mkuu wa 2025, ni dhahiri kwamba vyombo vya habari nchini vinakabiliwa na changamoto kubwa katika kuimarisha ubora wa uripoti. Mazingira ya muundo yanayozunguka vyombo vya habari lazima yabadilike ili kukuza nafasi ya wazi zaidi katika misingi ya usawa na haki kuhusu mustakabali wa baadaye wa nchi. Bila mabadiliko makubwa katika utendaji wa vyombo vya habari na muktadha mpana wa kisheria na kisiasa, kufikia maendeleo yenye maana katika kuripoti uchaguzi na ushiriki wa raia utabaki kwenye mkwamo mkubwa.

# 15.0 Mapendekezo

Kutokana na matokea ya utafiti, tunapendekeza yafuatayo:

Uhuru wa vyombo vya habari: Wadau wa vyombo vya habari wanapaswa kuwa imara katika kutetea uhuru wa vyombo vya habari, kutambua jukumu lake muhimu katika kukuza uwazi na uwajibikaji wa jamii. Hii inajumuisha kupinga waziwazi na kwa nguvu zote majaribio yoyote yanayoletwa na nguvu kutoka nje—mamlaka za kiserikali, wamiliki wa vyombo vya habari, vyama vya siasa au wagombea—kujaribu kuchezea au kushawishi mabadiliko ya maudhui kwa namna iliyo kinyume na maslahi ya umma. Ili kujihakikishia kunakuwa na vyombo vya habari vyenye uhuru wa kweli, wadau wanapaswa kutumia njia yenye sura nyingi. Hii ni pamoja na kutetea na kupambania uwepo mifumo thabiti ya kisheria ambayo inalinda waandishi wa habari kutokana na udhibiti na vitisho na kukuza mazingira ambapo uripoti wa masuala muhimu unaweza kustawi. Juu ya hayo yote, kuulinda uhuru wa vyombo vya habari ni wajibu wa pamoja na ambao unahitaji juhudi za pamoja kutoka kwa wadau wote, ili kuhakikisha kwamba vyombo vya habari vinaweza kutimiza jukumu lake muhimu katika kulinda demokrasia na kuimarisha ustawi wa jamii nchini.

Kwenda mbali zaidi katika uripoti: vituo vya redio na vyombo vingine vya habari vinapaswa kuzingatia zaidi masuala muhimu katika kampeni za uchaguzi kuliko kuripoti juujuu tu. Vyombo vya habari pia vinapaswa kuimarisha ubora wa uripoti wao kwa kwenda mbali zaidi na kuripoti kuhusu sera huku wakirejelea ilani za uchaguzi za vyama, kuuliza maswali magumu (au kutafuta vyanzo vya habari vyenye uwezo wa kufanya hivyo), hasa kuhusu mafanikio ya wagombea na kushindwa kwao. Jambo hili ni muhimu mno kwani linaongeza thamani ya uripoti na linawasaidia wananchi, ambao ndio wapiga kura wenyewe, kupata taarifa muhimu.

Mafunzo: wakati tukielekea kwenye Uchaguzi Mkuu baadae mwaka huu, na kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana kwenye uripoti wa vituo vya redio kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024 pamoja na changamoto ambazo waandishi wa habari walikumbana nazo, kuna haja ya kuandaa mafunzo ya muda mrefu ambayo yatazingatia hali halisi kama hiyo na waandishi wa habari ambao wameonyesha uwezo tu au ambao wana uzoefu wa awali wa kuripoti uchaguzi, watapaswa kushiriki katika mafunzo hayo. Mafunzo yanaweza yakaandaliwa kitaifa na mashirika ya misaada kwa vyombo vya habari au katika vyombo vya habari. Mafunzo hayo yanapaswa kuanza mapema zaidi ili kuwaandaa waandishi wa habari kuandika kwa ufanisi mizunguko yote mitatu ya uchaguzi. Baadhi ya shughuli za mzunguko wa kwanza kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kwa sasa zinaendelea, ikiwa ni pamoja na kuhuisha daftari la wapiga kura.

Orodha ya vitu vya kuripoti wakati wa uchaguzi: Ili kurahisisha kazi ya waandishi wa habari na wahariri, tunapendekeza kwamba vyumba vya habari vichapishe orodha ya bango la ukurasa mmoja litakalohusu jinsi ya kuripoti uchaguzi na kuliweka kwenye kuta za chumba chao cha habari kila mmoja alione kwa urahisi na waandishi wao kulifanyia marejeleo.

Bajeti kwa ajili ya kuripoti uchaguzi: kuripoti uchaguzi kunahitaji bajeti, wakati vyombo vya habari vikijipapatua kifedha ili kujiendesha, tunapendekeza kwamba wadau wa vyombo vya habari wazingatie kutenga fedha kwa ajili ya kuripoti uchaguzi. Akaunti maalumu au mfuko maalumu unapaswa kuandaliwa ili kuwalinda waandishi wa habari dhidi ya mitego ya vyama na wagombea wakati wa kipindi muhimu cha uchaguzi.

Kwa ujumla, tunapendekeza kwamba vyombo vya habari vinapaswa kuuendeleza na kuukumbatia utamaduni wa kuwa mlinzi mwangalizi (watchdog) katika jamii. Wanapaswa kujenga maadili na kaida za kitamaduni ili kuimarisha demokrasia, utawala wa sheria, na utawala wa jamii.


# YEARBOOK ON MEDIA QUALITY IN TANZANIA SINCE 2017


YEARBOOK ON MEDIA QUALITY IN TANZANIA SINCE 2017
















# Ziko wapi sauti za wagombea na wananchi?

## UCHUNGUZI WA URIPOTI WA VITUO VYA REDIO KUHUSU UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2024 NCHINI TANZANIA



HEKIMA NI UHURU

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
Shule Kuu ya Uandishi wa Habari
na Mawasiliano kwa Umma
S.L.P 4067 Mikocheni B Makaburi Street,
Plot Block D, No.34
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2700756
Barua pepe: sjmc@udsm.ac.tz
Tovuti: www.udsm.ac.tz

YEARBOOK ON MEDIA QUALITY IN TANZANIA
YBMQ

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra
**Embassy of Switzerland in Tanzania**

UK International Development
Partnership | Progress | Prosperity